JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2023

# URAIA NA MAADILI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA KUMALIZA ELIMU YA MSINGI (PSLE) 2023

# URAIA NA MAADILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO


DIBAJI .................................................................................................. iv

1.0 UTANGULIZI ..................................................................................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI 3

2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi .................................. 3

2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi ............................................ 76

3.0 HITIMISHO ........................................................................................ 98

4.0 MAPENDEKEZO ................................................................................ 99

KIAMBATISHO: Ulinganifu wa Ufaulu kwa Watahiniwa kwa kila Umahiri katika Mtihani wa PSLE 2022 na 2023 ......................................... 100

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa Taarifa ya Uchambuzi wa Majibu ya Watahiniwa (CIRA) wa Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) mwaka 2023. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho kwa walimu, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani huu. Mtihani wa Uraia na Maadili uliandaliwa kwa lengo la kutahini umahiri wa watahiniwa na ufanisi uliofikiwa katika kutekeleza muhtasari wa somo kuanzia Darasa la III - VII. Hii ni kwa sababu ubora wa majibu ya watahiniwa katika mtihani ni miongoni mwa viashiria vinavyoonesha kuwa watahiniwa waliweza/hawakuweza kujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka saba ya elimu ya msingi.

Uchambuzi umeonesha kuwa watahiniwa waliokuwa na ufaulu mzuri walikuwa na umahiri wa kutosha katika dhana zilizopimwa na uwezo mzuri wa kuelewa maswali na kujibu kwa ufasaha. Kwa upande mwingine, watahiniwa walioshindwa kujibu maswali kwa usahihi walikosa umahiri wa kutosha katika dhana zilizotahiniwa, kushindwa kuelewa vema maswali husika na kushindwa kufuata maelekezo ya mtihani. Kwa ujumla ufaulu wa watahiniwa katika somo hili ulikuwa wa wastani.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina matumaini kuwa mrejesho uliotolewa katika taarifa hii utatoa picha halisi kwa wadau wote wa elimu kuhusu changamoto wanazokumbana nazo watahiniwa katika kujibu maswali ya mtihani na namna ya kuzitatua ili kuongeza ufaulu katika mitihani ijayo.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, wataalamu wa TEHAMA na wengine wote walioshiriki kuandaa taarifa hii.

Dkt. Said A. Mohamed
**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mitihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) 2023 kwa somo la Uraia na Maadili ulipima umahiri ulioainishwa katika muhtasari wa somo la Uraia na Maadili wa mwaka 2019 kwa Darasa la III - VII na umezingatia fomati ya mtihani ya mwaka 2020. Karatasi ya mtihani ilikuwa na maswali 45 yaliyogawanyika katika Sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali 40 ya kuchagua jibu sahihi na Sehemu B ilikuwa na maswali matano (5) ya majibu mafupi. Mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kutoka katika kila sehemu. Kila swali katika Sehemu A lilikuwa na alama moja (1) na hivyo kufanya jumla ya alama 40. Katika Sehemu B, kila swali lilikuwa na alama mbili (2) na kufanya jumla ya alama 10 katika sehemu hii. Hivyo, mtihani mzima ulikuwa na jumla ya alama 50.

Jumla ya watahiniwa 1,397,293 waliandikishwa kufanya mtihani. Kati yao, watahiniwa 1,356,306 (97.07%) walifanya mtihani. Watahiniwa 40,987 (2.93%) hawakufanya mtihani kutokana na sababu mbalimbali kama vile utoro na kuugua kwa muda mrefu. Uchambuzi wa takwimu za ufaulu za watahiniwa zinaonesha kuwa watahiniwa 1,113,694 (82.12%) waliufaulu kwa kupata madaraja (A, B, na C) wakati watahiniwa 242,534 (17.88%) walifeli kwa kuwa walipata madaraja (D-E).

Katika sehemu A, uchambuzi wa majibu ya watahiniwa ulifanyika kwa mujibu wa machaguo yao ambayo ni A, B, C, D na E. Sababu zilizosababisha mtahiniwa kufanya kila chaguo kwa kila swali zimeainishwa. Herufi ya jibu sahihi imewekewa alama ya nyota (*) katika majedwali na chati kwa ajili ya maelekezo. Aidha, asilimia ya watahiniwa ambao hawakufuata maelekezo ya namna ya kujibu swali iliwekwa katika uchambuzi na kupewa jina “mengine” kama inavyoonekana katika majedwali na chati.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika sehemu B ulijikita katika kuangalia ubora wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa na ufaulu katika swali husika. Vielelezo vinavyoonesha majibu mazuri na mabaya vimetumika kuonesha ubora wa majibu yaliyotolewa na watahiniwa. Takwimu za ufaulu wa watahiniwa katika kila swali zimewasilishwa kwa kutumia Chati. Muhtasari wa viwango vya

ufaulu kwa kila mada umeoneshwa katika Kiambatisho kilichopo mwishoni mwa taarifa hii.

Ufaulu wa watahiniwa katika kila swali umegawanywa katika viwango vitatu: *vizuri*, *wastani* na *hafifu*. Viwango hivi vimetokana na asilimia ya watahiniwa waliofaulu katika swali husika. Ikiwa watahiniwa waliofaulu swali ni asilimia 60 – 100, 40 – 59 na 0 – 39 ufaulu huo ni mzuri, wastani na hafifu, mtawalia.


## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi

**Swali la 1:** Uhuru na umoja wa kitaifa ni mambo ya kujivunia kwa kila mtanzania. Ipi ni athari inayotokana na kuvurugwa kwa uhuru na umoja wa taifa nchini?

A Kudumaa kwa maendeleo ya nchi
B Kupungua kwa deni la Taifa
C Kupungua kwa vitega uchumi
D Kukosekana kwa utawala bora
E Kuongezeka kwa rushwa

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na liliwataka watahiniwa kubaini athari za kuvurugwa kwa uhuru na umoja wa kitaifa nchini. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306. Watahiniwa 436,244 (32.16%) walijibu kwa usahihi ambapo watahiniwa 920,062 (67.84%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kudumaa kwa maendeleo ya nchi* walielewa athari zinazohusiana na kuvurugwa kwa Uhuru na umoja wa kitaifa nchini. Athari zilizobainishwa ni kama vile ukosefu wa huduma nzuri za afya, usambazaji duni wa maji safi na salama, elimu duni ya uraia, kipato duni na lishe duni. Vilevile, madhara mengine ni kuporomoka kwa demokrasia, kukosa utulivu wa kisiasa na kijamii, kushuka kwa uchumi, kushuka kwa heshima kimataifa, na athari za kisaikolojia na kihisia. Chati Na 1 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 1.





**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 1*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 57,178 (4.22%) waliochagua jibu lisilo sahihi B, *Kupungua kwa deni la Taifa*, hawakutambua kwamba kupungua kwa deni la taifa ni athari chanya itokanayo na kudumisha uhuru na umoja wa kitaifa. Walipaswa kutambua kuwa ikiwa uhuru na umoja wa kitaifa utavurugwa, kutatokea machafuko ya kijamii, kisiasa na kiuchumi ambavyo hatimaye huathiri mtiririko wa mapato ya nchi ambayo yangetumika katika matumizi mbalimbali ya serikali kama vile kulipa madeni ya taifa na kugharamia huduma za kijamii. Vilevile, watahiniwa 68,467 (5.05%) waliochagua kipotoshi C, *Kupungua kwa vitega uchumi,* watahiniwa 472,577 (34.84%) waliochagua kipotoshi D, *Kukosekana kwa utawala bora* na 306,632 (22.61%) waliochagua kipotoshi E, *Kuongezeka kwa rushwa* hawakuwa sahihi kwa sababu machaguo yote C, D, na E ni viashiria vya nyanja mbalimbali za maendeleo duni ya nchi. Kwa mfano, chaguo C, *Kupungua kwa vitega uchumi* limejikita katika athari za kiuchumi tu, na pia vipotoshi D, *Kukosekana kwa utawala bora* na E, *Kuongezeka kwa rushwa,* vinaonesha athari za kisiasa na kijamii za kuvurugwa kwa uhuru na umoja wa kitaifa.

**Swali la 2:** Watu wenye mahitaji maalumu hujisikia vizuri na kujiamini wanapopendwa na kuthaminiwa katika jamii. Ni tendo gani linapaswa kuepukwa tunapotoa huduma kwa watu wa kundi hilo?

A Kuwapa huduma sahihi za afya
B Kuwachagua katika nafasi za siasa
C Kuwatenga kwenye nafasi za uongozi
D Kuwasaidia kwenye masuala ya kisheria
E Kutumia lugha vizuri

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu dhana ya kujipenda na kuwapenda watu wengine hasa wenye mahitaji maalumu katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 917,613 (67.66%) walijibu kwa usahihi ikilinganishwa na watahiniwa 438,693 (32.34%) waliojibu isivyo sahihi. Jibu sahihi lilikuwa C, *Kuwatenga kwenye nafasi za uongozi* ambalo lilichaguliwa na watahiniwa waliokuwa na uelewa wa watu wenye mahitaji maalumu kuwa ni watu wenye ulemavu au hali ya kuhitaji msaada ili waweze kushiriki kikamilifu katika nyanja mbalimbali za maisha. Hii inaweza kujumuisha walemavu wa viungo, akili, udumavu wa akili, uzee, utoto na ualbino. Vilevile walielewa kuwa wakati wa kuchangamana na watu wenye mahitaji maalumu ni muhimu kuwatendea heshima, huruma na kuwajali. Kwa muktadha huu, watahiniwa walibainisha matendo ya kuepukwa wakati wa kuwahudumia wenye mahitaji maalum kama kuwabagua kwenye nafasi za uongozi, kutumia lugha ya dhihaka, kuwakejeli, kuwazira na kuwafanyia ukatili wa kimwili au maneno. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 2.




**Chati Na. 2***: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 2*


Hata hivyo, watahiniwa 168,566 (12.43%) waliochagua kipotoshi A, *Kuwapa huduma sahihi za afya*, 119,162 (8.79%) waliochagua kipotoshi B, *Kuwachagua katika nafasi za siasa*, 71,276 (5.26%) waliochagua kipotoshi D, *Kuwasaidia kwenye masuala ya kisheria* na 67,793 (5.00%) waliochagua kipotoshi E, *Kutumia lugha vizuri*, hawakuwa na uelewa kuhusu matendo yanayowabagua watu wenye mahitaji maalumu katika kushiriki kwenye shughuli mbalimbali za kijamii. Vipotoshi A, B, D na E vilijumuisha matendo yanayoonesha kuwapenda na kuwathamini watu wenye mahitaji maalumu katika jamii. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi A, *Kuwapa huduma sahihi za afya*, walitakiwa kuelewa kwamba watu wenye mahitaji maalumu wanahitaji kupata huduma stahiki zinazohusiana na kuimarisha afya zao ili waweze kushiriki katika kazi za kijamii na kiuchumi. Waliochagua kipotoshi B, *Kuwachagua kwenye nafasi za siasa* hawakuelewa kwamba watu wenye mahitaji maalumu wanastahili kufurahia haki zao ikiwemo haki ya kupiga na kupigiwa kura katika nafasi mbalimbali za uongozi wa kisiasa. Vile vile, watahiniwa waliochagua kipotoshi D, *Kuwasaidia kwenye masuala ya kisheria* hawakuelewa kwamba watu wenye mahitaji maalumu huhitaji msaada wa kisheria pindi wanapopata changamoto mbalimbali kama vile mashitaka ya kubambikiwa kesi, unyanyasaji wa kingono, dhuluma katika mirathi kwa kutaja machache tu. Msaada wa kisheria kama huo, mara nyingi, hutolewa bure na watu binafsi,

taasisi na wanasheria wa serikali. Huduma nyingine zitolewazo kwa watu wenye mahitaji maalumu hujumuisha huduma za afya, ushauri na mahitaji muhimu ya kibinadamu kama vile chakula, malazi na mavazi. Watahiniwa waliochagua kipotoshi E, *Kutumia lugha vizuri,* hawakuelewa kwamba lugha inayostahili kutumika kwa watu wa kundi kama hili inatakiwa kuakisi hisia za huruma, moyo wa upendo na mapenzi kwao ili wajisikie kuwa wanapendwa na kuthaminiwa katika jamii. Kwa hiyo, chaguo hili lisingeweza kuwa miongoni mwa matendo ya kuepukwa wakati wa kuwahudumia watu wenye mahitaji maalumu.

**Swali la 3:** Wanafunzi wanapaswa kushirikishwa katika mchakato wa kupanga mipango ya maendeleo ya shule zao. Ni kipengele gani kinapaswa kuonekana kabla ya vingine katika mpango mkakati wa shule?

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| A | Tathmini | B | Muda | C | Utekelezaji |
| D | Malengo | E | Mahitaji | | |

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu vipengele na taratibu zinazohusika katika kuandaa mpango mkakati wa shule. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 573,155 (42.26%) walijibu kwa usahihi ikilinganishwa na watahiniwa 783,151 (57.74%) walioshindwa kujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliokuwa na uelewa walichagua jibu sahihi D, *Malengo*. Watahiniwa hao walielewa kuwa malengo ni mipango mahususi inayoweza kupimika ambayo mtu binafsi au shirika linalenga kufikia ndani ya muda fulani. Kwa hiyo, lengo ni jambo la kwanza kuzingatia wakati wa kupanga kwa ajili ya hatua yoyote kwa sababu hutoa mwelekeo, na ni msingi wa kufanya uamuzi. Vilevile, malengo huongeza motisha, hukuza uwajibikaji, huokoa muda, hujenga imani ya mtu binafsi na hufanya yasiyoonekana kuonekana. Chati Na 3 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Kwa upande mwingine, kipotoshi A, *Tathmini* kilichaguliwa na watahiniwa 237,940 (17.54%) ambao hawakuwa na ufahamu wa vipengele na hatua za uandaaji wa mpango mkakati. Walishindwa kuelewa kwamba tathmini inahusisha kupima ufanisi na matokeo ya programu husika, ikiwa ni pamoja na mipango na mikakati ya jumla. Inabainisha iwapo mpango unafikia malengo yake na kwa kutambua maeneo ambayo yanaweza kuhitaji uboreshaji au marekebisho. Hivyo, tathmini inapaswa kuwa sehemu ya mwisho ya kuzingatiwa wakati wa kuandaa mpango mkakati wa shule

Zaidi ya hayo, watahiniwa 194,896 (14.37%) waliochagua jibu lisilo sahihi B, *Muda* hawakuwa na ufahamu kwamba muda ni wakati ambao mpango mkakati unatekelezwa na malengo yanafikiwa. Muda ni muhimu kwa sababu husaidia watu/taasisi husika kukaa kwenye mstari na kutanguliza juhudi zake. Pia, unahakikisha kwamba mpango mkakati unawiana na maono na malengo ya muda mrefu ya mtu au taasisi.


Vilevile, watahiniwa 182,101 (13.43%) waliochagua kipotoshi C, *Utekelezaji* hawakufahamu kuwa utekelezaji ni mojawapo ya kipengele kinachorejelea mchakato wa kuweka mpango mkakati katika vitendo. Unahusisha kutafsiri malengo ya mpango katika hatua na mipango madhubuti, kugawa rasilimali na kuhakikisha kuwa mpango unatekelezwa kwa ufanisi. Huamua jinsi

mpango mkakati utakavyofanikiwa kufikia malengo yake. Pia, husaidia watu/shule/taasisi kuwajibika kwa matendo yake na kuonesha dhamira yake ya kuboresha kila mara. Kwa maana halisi, kipengele hiki ni cha nne baada ya kubainisha lengo, kuweka muda na rasilimali za kuhamasisha. Mwisho, watahiniwa 152,700 (11.26%) walishindwa kuelewa kuwa mahitaji ni pamoja na rasilimali kama vile watu, fedha na zana, ambazo hutumika kufikia malengo. Watahiniwa hawakufahamu kuwa baada ya kuweka malengo na muda wa mpango kazi, jambo la tatu ni kukusanya rasilimali kulingana na mahitaji ya mpango mkakati.

**Swali la 4:** Ni kiongozi yupi katika muundo wa serikali ya kata ana kazi na wajibu wa kuelimisha jamii dhidi ya tamaduni potofu?

A Diwani
B Afisa maendeleo
C Afisa mtendaji
D Afisa elimu
E Afisa afya

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa wa kuelewa muundo wa serikali za mitaa katika ngazi ya kata na majukumu ya viongozi katika ngazi hiyo. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 364,618 (26.88%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 991,688 (73.12%) walishindwa kujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi B, *Afisa maendeleo* walikuwa wanafahamu majukumu na wajibu wa Afisa Maendeleo katika Kata; kwamba yeye ni Afisa ambaye ana jukumu la kuwezesha na kukuza mipango ya maendeleo ya jamii. Majukumu mengine ni kama vile kupinga tamaduni zilizopitwa na wakati, kusimamia na kuratibu shughuli za maendeleo katika Kata, kuelimisha watu kuhusu umuhimu wa lishe bora, uhifadhi wa mazingira na kutoa mafunzo na programu za kujenga uwezo. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 4*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 299,309 (22.07%) waliochagua kipotoshi A, *Diwani* hawakujua kwamba diwani ni mwakilishi aliyechaguliwa na wananchi wa kata husika. Anahudumu kama mjumbe wa baraza la mtaa/kijiji katika kata yake. Majukumu yake ni pamoja na kuwakilisha maslahi na kero za wakazi wa kata yake, kushiriki katika uamuzi, kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo, na kuhakikisha utawala bora na utoaji wa huduma bora ndani ya eneo lake la utawala.

Pia, watahiniwa 233,572 (17.22%) waliochagua kipotoshi C, *Afisa mtendaji* hawakujua kuwa ni kiongozi wa utawala anayehusika na usimamizi wa kila siku wa shughuli za kiuchumi na kijamii katika serikali za mitaa. Majukumu yake ni pamoja na kutekeleza sera na programu mbalimbali, kusimamia huduma za umma, kusimamia fedha, rasilimali na kuhakikisha utoaji wa huduma kwa ufanisi.


Vilevile, watahiniwa 304,894 (22.48 %) waliochagua kipotoshi D, *Afisa elimu*, hawakuwa na uelewa kuwa Afisa elimu ndiye mwenye dhamana ya kusimamia masuala ya elimu ndani ya eneo la serikali ya kata yake. Anawajibika kusimamia taasisi za elimu, kutekeleza sera na programu za elimu, kufuatilia utendaji wa kitaaluma, kutoa msaada na mwongozo kwa walimu, na kuhakikisha elimu bora inapatikana kwa wote.

Aidha, watahiniwa 137,201 (10.12%) waliochagua kipotoshi E, *Afisa Afya* hawakujua kuwa afisa wa afya ana wajibu wa kusimamia huduma za afya ndani ya eneo la lake. Pia, hawakujua kuwa anawajibika kutekeleza sera na programu za afya, kuratibu huduma za afya, kusimamia vituo vya afya, kukuza afya ya umma na hatua za kinga na kuhakikisha utoaji wa huduma bora za afya.

**Swali la 5:** Kila shule inahitaji kufanya vizuri kitaaluma. Ni njia ipi inaweza kuisaidia shule kufanya vizuri kitaaluma?

A Kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi shuleni
B Kuwa na wanafunzi wenye nidhamu
C Kuwa na idadi kubwa ya watumishi shuleni
D Kuwaruhusu walimu kushiriki kazi za nje muda wote
E Kufanya midahalo mara kwa mara shuleni

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa wa kubaini njia ambazo zinaweza kuboresha ufaulu wa wanafunzi shuleni. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 986,154 (72.71%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 370,152 (27.29%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Kuwa na wanafunzi wenye nidhamu,* walitambua aina ya utovu wa nidhamu ambao unaweza kusababisha ufaulu duni katika masomo. Utovu huo wa nidhamu ni pamoja na utoro, kukosa heshima, uonevu, udanganyifu, matumizi ya dawa za kulevya, uharibifu, mapigano, lugha zisizofaa na ukiukaji wa maadili ya mavazi. Mambo yote haya husababisha ufaulu duni katika masomo. Aidha, watahiniwa hawa walifahamu njia zinazosaidia kufanya vizuri kitaaluma; baadhi ya njia hizo ni pamoja na mahusiano chanya, usimamizi wa muda, kuweka malengo, ujuzi wa kutatua matatizo, kujistahi zaidi, heshima kwa mamlaka, na uwezo wa kufanya uamuzi sahihi. Kwa ujumla, kuboresha utendaji wa kitaaluma shuleni kunahitaji mbinu nyingi. Baadhi ya mbinu ambazo shule zinaweza kutumia ni pamoja na kuwa na uongozi bora, kuwa na ufundishaji wa hali ya juu, kuwa na ushirikishwaji wa wazazi/walezi; kuwa na matumizi ya teknolojia sahihi. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 5.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 52,619 (3.88%) waliochagua kipotoshi A, *Kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi shuleni* na watahiniwa 44,020 (3.25%) waliochagua kipotoshi C, *Kuwa na idadi kubwa ya watumishi shuleni* hawakujua kuwa idadi kubwa ya watu shuleni sio kigezo cha kufanya vizuri kitaaluma kwa kuwa wanafunzi wana tabia mbalimbali nzuri na mbaya. Kwa hivyo, kuwa na wanafunzi wengi shuleni wenye tabia mbaya hakusaidii kufanya vizuri kitaaluma. Kadhalika, idadi kubwa ya watumishi shuleni haisaidii kufanya vizuri kitaaluma ikiwa wanafunzi hawana nidhamu.

Aidha, watahiniwa 49,845 (3.68%) waliochagua kipotoshi D, *Kuwaruhusu walimu kushiriki kazi za nje muda wote*, hawakuwa sahihi kwa kuwa shughuli za ziada au za nje ni zile shughuli ambazo si sehemu ya ratiba ya masomo ya shule ya kila siku. Hawakujua kuwa walimu hawatapata muda wa kutosha wa kuwasaidia wanafunzi katika masuala ya kitaaluma.


Pia, watahiniwa 211,683 (15.61%) waliochagua kipotoshi E, *Kufanya midahalo mara kwa mara shuleni* hawakuwa sahihi kwa sababu mijadala ya mara kwa mara ya masomo au umahiri tofauti shuleni unaweza usisaidie kuinua ufaulu wa shule ikiwa wanafunzi hawana nidhamu. Vilevile, mijadala inaweza isiwe ya kitaaluma, kwa mfano Wakristo na

Waislamu, mijadala juu ya uhalifu ambayo haichangii chochote katika kufanya vizuri kitaaluma.

**Swali la 6:** Ipi kati ya zifuatazo ni sifa nzuri ya shule?

A Wanafunzi kupewa muda mwingi wa kucheza
B Walimu kuonesha nidhamu nzuri
C Viongozi wa shule kuwa na uhuru mkubwa
D Kutunzwa vizuri kwa mazingira ya shule
E Wanafunzi kuvaa sare wanazozipenda

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kutambua sifa nzuri za shule. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 791,210 (58.34%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 565,096 (41.66%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Kutunzwa vizuri kwa mazingira ya shule* walijua kuwa shule nzuri ina sifa ya kuwa na mazingira yaliyohifadhiwa. Sifa nyingine ni pamoja na walimu wenye taaluma na wanaojitolea, mazingira salama, uongozi imara, kuwa na matarajio makubwa, kuwa na mahusiano chanya, uwepo na mawasiliano bora na fursa za ziada. Chati Na. 6 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 6*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 52,315 (3.86%) waliochagua kipotoshi A, *Wanafunzi kupewa muda mwingi wa kucheza* na watahiniwa 66,145 (4.88%) waliochagua kipotoshi E, *Wanafunzi kuvaa sare wanazozipenda* hawakuwa sahihi kwa kuwa kuwapa wanafunzi muda mwingi kucheza kunaweza kudumaza ufaulu wa shule kwani baadhi yao wanaweza kushindwa kuleta uwiano kati ya kucheza na kusoma kinyume na malengo ya msingi ya shule. Zaidi ya hayo, watahiniwa hao hawakujua kuwa kuruhusu wanafunzi kuvaa sare wanazozipenda kunaweza kuhimiza uvaaji usio na staha miongoni mwa wanafunzi ambapo sifa ya shule inaweza kuharibika.


Aidha, watahiniwa 391,518 (28.87%) waliochagua kipotoshi B, *Walimu kuonesha nidhamu nzuri,* walifahamu dhima kuu ya walimu wenye nidhamu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji lakini walishindwa kubainisha sifa nzuri za shule kama jumla ya mambo yote shuleni na si masuala machache tu katika jumuiya ya shule. Walimu wanaweza kuwa na nidhamu (upande wao) lakini kwa upande wa walengwa (wanafunzi) wasiwe na nidhamu; hivyo nidhamu ya walimu si kigezo pekee cha kufanya vizuri kitaaluma shuleni. Pia, watahiniwa 42,870 (3.16%) waliochagua kipotoshi C, *Viongozi wa shule kuwa na uhuru mkubwa* hawakujua ukweli kwamba shule zinaongozwa na sheria na kanuni; viongozi na watumishi wengine walio chini yao wanatarajiwa kuzingatia sheria na kanuni hizo. Kwa hivyo, suala la uhuru kamili halijitokezi na haliwezi kutumika kuashiria shule bora ikiwa sheria na kanuni husika hazifuatwi.

**Swali la 7:** Kwa nini wanafunzi wanashauriwa kuvaa vizuri na kuwa nadhifu shuleni na nyumbani?

A Ili kuakisi utandawazi
B Ili kuonesha usasa
C Ili kuakisi tabia njema
D Ili kuonesha mitindo ya mavazi
E Ili kuonesha ufahari

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu jamii* na liliwataka watahiniwa kubainisha sababu za wanafunzi kuvaa vizuri na kuwa nadhifu shuleni na nyumbani. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,040,450 (76.71%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 315,856 (23.29%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Ili kuakisi tabia njema*, walielewa

kwamba kuvaa vizuri kunamaanisha kuvaa nguo zinazofaa kwa muktadha, safi, zenye kushonwa vizuri na zenye kuakisi utamaduni wa jamii husika. Pia, kuvaa vizuri shuleni na nyumbani kunaonesha maadili mema kwa kuwa aina ya uvaaji unaakisi tabia ya mtu husika. Zaidi ya hayo, kuvaa vizuri shuleni na nyumbani ni muhimu kwa sababu hukuza nidhamu, usawa, huongeza umakini, hujenga taaluma, usalama na hisia chanya. Chati Na. 7 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 7.




**Chati Na. 7**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 7*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 99,485 (7.33%) waliochagua kipotoshi A, *Ili kuakisi utandawazi* pamoja na watahiniwa 51,807 (3.82%) waliochagua kipotoshi B, *Ili kuonesha usasa,* hawakuwa sahihi, kwa sababu utandawazi umesababisha kuenea kwa baadhi ya mitindo hasi ya kisasa ya uvaaji wa kimagharibi na usasa wakati mwingine ni kinyume na maadili ya kitamaduni yanayokubalika katika jamii zikiwemo shule.


Vivyo hivyo, watahiniwa 78,045 (5.75%) waliochagua kipotoshi D, *Ili kuonesha mitindo ya mavazi* hawakuwa sahihi kwa sababu wazazi/walezi wanaowajibika wanatarajiwa watoto wao wafuate kanuni zinazofaa za mavazi/uvaaji. Kwa jambo hilo, mtindo wa uvaaji hauwezi kutumika kama kiashiria cha tabia njema. Mwisho, watahiniwa 74,756 (5.51%) waliochagua kipotoshi E, *Ili kuonesha ufahari,* pia hawakuwa sahihi kwa kuwa kuvaa

vizuri na kuwa nadhifu si kuwa na heshima, hadhi au pongezi kwa sababu ya kuvaa mavazi ya gharama badala yake, watu wanakusudia kuonesha tabia ifaayo katika jamii wanamoishi.

**Swali la 8:** Ni shughuli ipi kati ya zifuatazo **sio** ya kujitolea?

A Kuanzisha bustani za mboga
B Kufagia eneo la shule
C Kushiriki katika klabu ya skauti
D Kupanda miti au maua shuleni
E Kuimba wimbo wa shule

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu jamii* na lililenga kupima uwezo wa watahiniwa kutambua shughuli za hiari na zisizo za hiari. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 601,982 (44.38%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 754,324 (55.62%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi E, *Kuimba wimbo wa shule* walielewa kuwa hiyo ni mojawapo ya shughuli zinazohitaji ulazima katika muktadha maalumu. Wimbo wa shule ni mojawapo ya alama za shule ambayo hufanya shule fulani kutambuliwa kati ya nyingine. Kwa sababu hiyo, kuimba wimbo wa shule siyo hiyari ni lazima kwa wanafunzi wote. Shughuli nyingine zisizo za hiyari shuleni ni pamoja na kuhudhuria shule, kuvaa sare za shule, kufanya majaribio/mitihani, na kushiriki katika shughuli za ziada. Chati Na. 8 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 8.




**Chati Na. 8**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika swali la 8*


Kwa upande mwingine, watahiniwa 266,111 (19.62%) waliochagua kipotoshi A, *Kuanzisha bustani za mboga,* hawakujua kuwa kuanzisha bustani ya mboga kama sehemu ya shughuli za kujitegemea ambayo wanafunzi huchagua kufanya bila kuhitajika au kulipwa fidia. Uanzishwaji wa bustani ya mboga mboga hukuza ujuzi wa vitendo wa wanafunzi na huchochea hamu ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji kwa hiari.

Aidha, watahiniwa 87,538 (6.45%) waliochagua kipotoshi B, *Kufagia eneo la shule*, na watahiniwa 64,316 (4.74%) waliochagua kipotoshi D, *Kupanda miti au maua shuleni*, hawakuwa sahihi kwa sababu inatarajiwa wanafunzi kwa hiari yao wawe wenye kujitolea kufanya usafi na kutunza mazingira ya shule ili yapendeze ili kuvutia na kuweka hali nzuri ya mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji. Vilevile, watahiniwa 320,097 (23.60%) waliochagua kipotoshi C, *Kushiriki katika klabu ya skauti* hawakuwa sahihi kwa sababu kuanzisha na kujiunga na vilabu vya skauti ni hiari kwa wanafunzi. Lengo la klabu ya skauti ni kusaidia kuwafanya wanafunzi wawe na nguvu ya kufanya kazi, wawe wenye kustahimili baadhi ya changamoto, wawe na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na uzalendo miongoni mwao. Kwa hivyo, watahiniwa waliochagua majibu yasiyo sahihi hawakuweza kubainisha tofauti kati ya shughuli za hiari na zisizo za hiari.

**Swali la 9:** Utakiitaje kitendo cha vijana wengi kushiriki katika majanga ya moto kwa kusaidia kutokuteketea kwa watu, mifugo, majengo na vifaa vingine?

A Zimamoto B Uokoaji C Uhodari
D Uzalendo E Utiifu

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini jamii* na lilipima uwezo wa watahaniwa wa kubainisha istilahi sahihi ya tendo la jamii kukabili majanga na uokoaji kwa wahanga. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 kati yao 748,329 (55.17%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 607,977 (44.82%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua chaguo sahihi *B, Uokoaji* walifahamu kuwa ni kitendo cha kumtoa mtu katika hatari kutokana na madhara, au hali hatarishi. Uokoaji unaweza kufanywa na watu binafsi, mashirika au timu maalumu kama vile kikosi cha uokoaji. Uokoaji unahusiana moja kwa moja na kuokoa maisha na kupunguza madhara katika dharura. Chati. Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 9.




**Chati Na. 9**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 9.*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 287,212 (21.18%) waliochagua kipotoshi A, *Zimamoto* hawakuwa sahihi kwa sababu inarejelea timu maalumu au kikundi cha watu waliofunzwa, ambao mara nyingi hujumuisha

wataalamu wa zimamoto na washiriki wengine wa huduma ya kwanza. Timu hiyo ina vifaa vya kushughulikia matukio mbalimbali ya dharura, kama vile moto, dharura za matibabu, ajali za magari, uokoaji wa maji na zaidi. Vikosi vya uokoaji vina jukumu muhimu katika usalama wa umma kwa kukabiliana na dharura mbalimbali. Pia, kufanya kazi za kuokoa maisha, na kudumisha usalama kwa jamii nzima. Watahiniwa 56,675 (4.18%) waliochagua kipotoshi C, *Uhodari* hawakujua kuwa humaanisha ushujaa, ubora au hali ya kuonesha nguvu za kiakili au kimaadili katika kukabiliana na hatari, hofu au ugumu ambao ni sifa mojawapo ya zimamoto lakini si kitendo cha kuzima moto.


Vivyo hivyo, watahiniwa 206,775 (15.25%) waliochagua kipotoshi D, *Uzalendo*, na 41,661 (3.07%) waliochagua kipotoshi E, *Utiifu* hawakuwa sahihi kwani vipotoshi vyote viwili havirejelei kitendo cha kuokoa watu na mali zao kutokana na janga la moto. Kwa hakika, uzalendo unarejelea hisia ya upendo, kujitolea, na hali ya kushikamana na nchi yako ambayo humsukuma raia anayewajibika kuwa tayari kutetea uhuru wa taifa lake, uhuru na utamaduni wake na kushiriki kikamilifu katika kufanya kazi kwa ajili ya jamii na taifa kwa ujumla. Mwisho, utiifu ni nidhamu au adabu ya tabia ambayo nayo haihusiani na kumtoa mtu au vitu katika hatari.

**Swali la 10**: Mahusiano mema katika jamii hujengwa kwa matendo mazuri yanayotendwa na wanajamii. Ni matendo gani yanajenga mahusiano hayo?

A Uaminifu na ubinafsi
B Uvivu na ustahimilivu
C Ukweli na uwazi
D Uaminifu na umbea
E Uvumilivu na migogoro

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uelewa wa watahiniwa wa kubaini matendo yanayofanyika katika jamii ambayo yanaleta uhusiano mazuri. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,121,147 (82.66%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 235,159 (17.34%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Ukweli na uwazi* walielewa kwamba ukweli ni sifa ya kuwa mnyoofu, sahihi, na ni uthibitisho wa jambo kama lilivyo. Aidha, uwazi unarejelea mawasiliano pasipo kificho, na uwajibikaji. Unasaidia kupunguza kutoelewana na migogoro. Ukweli na uwazi ni tunu muhimu zinazosaidia kujenga uaminifu na uelewano kati ya watu binafsi na vikundi katika jamii. Tunu hizi ni muhimu kwa ajili ya kukuza mahusiano

chanya na kukuza jamii yenye afya na utendaji kazi mzuri. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 10*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 97,294 (7.17%) waliochagua kipotoshi A, *Uaminifu na ubinafsi*, hawakuwa sahihi kwa sababu ubinafsi ni kitendo cha kutanguliza maslahi na matamanio ya mtu binafsi kuliko ya wengine. Unaweza kuwa na athari mbaya katika kujenga uhusiano mzuri kwa sababu unaweza kusababisha hisia za chuki na kutoaminiana miongoni mwa watu. Watu ambao ni wabinafsi wana uwezekano mdogo wa kujenga uhusiano imara na wa kudumu na watu wengine. Aidha, uaminifu ni sifa mojawapo ya kujenga mahusiano mazuri kwa sababu hujenga imani miongoni mwa watu na hukuza mawasiliano chanya, hivyo kuleta ushirikiano bora.

Vilevile, watahiniwa 51,719 (3.81%) waliochagua kipotoshi B, *Uvivu na ustahimilivu*, hawakuwa sahihi kwani uvivu ni hali ya kutotaka kufanya kazi au kuweka juhudi. Uvivu unaweza kuwa na madhara kwa mahusiano kwa sababu unasababisha ukosefu wa mchango na usaidizi. Mtu mvivu mara nyingi anaweza kusababisha kukosa usawa na kuzorota kwa uhusiano mzuri katika jamii. Pia, ustahimilivu ni uwezo wa kuhimili shida au vikwazo.

Ni sifa muhimu kwa ajili ya kujenga mahusiano mazuri kwa sababu inaonesha kujitolea kwa uhusiano kwa kufanya kazi kupitia changamoto mbalimbali.

Aidha, watahiniwa 37,932 (2.80%) waliochagua kipotoshi D, *Uaminifu na umbea*, hawakujua kuwa umbea ni masengenyo, ni kitendo cha kueneza uvumi au kuongelea mambo binafsi ya wengine. Ni tabia ya kutoa habari bila kutumwa. Unaweza kuwa na madhara katika mahusiano kwa kuwa unaweza kusababisha kutoaminiana na migawanyiko kati ya watu. Pia, unaweza kutengeneza mazingira ya sumu na kuharibu uhusiano ndani ya kikundi au jamii. Uaminifu huchangia mahusiano mazuri kwani watu wanapokuwa waaminifu wao kwa wao uwezekano wa kujihisi salama katika mahusiano yao unakuwa ni mkubwa.


Pia, watahiniwa 36,974 (2.73%) waliochagua kipotoshi E, *Uvumilivu na migogoro*, hawakuwa sahihi kwa kuwa migogoro ni kutoelewana au mabishano kati ya mtu na mtu, watu au vikundi. Ni hali ya kutoafikiana baina ya pande mbili au zaidi. Ikiwa migogoro haitashughulikiwa inaweza kusababisha uharibifu na kuvunjika kwa mahusiano ya kijamii. Uvumilivu ni uwezo wa kukubali na kuheshimu tofauti za wengine. Hivyo, ni sifa mojawapo inayojenga uhusiano mzuri katika jamii, kwa sababu inaruhusu watu kuishi pamoja na kushirikiana licha ya tofauti zao.

**Swali la 11**: Vitendo vya kikatili kwa watoto vinaweza kufanyika katika ngazi mbalimbali kwenye jamii. Je, mtoto anawezaje kuepuka vitendo hivyo?

A Kuwa mpole na mnyenyekevu
B Kuwa mwadilifu na mwangalifu
C Kuwa mpole na mcheshi
D Kuwa mchangamfu na mpole
E Kuwa mstahimilivu na mwadilifu

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* na liliwataka watahiniwa kubaini njia ambazo kwazo mtoto anaweza kuepuka vitendo vya kikatili vinavyofanyika katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 764,184 (56.34%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 592,122 (43.66%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Kuwa mwadilifu na mwangalifu*

walielewa kuwa vitendo vya kikatili ni aina yoyote ya unyanyasaji wa kimwili, kihisia, au kingono au kutelekezwa ambao husababisha madhara, majeraha, na hata dhiki. Vilevile, walijua baadhi ya madhara yanayoweza kumpata mtoto kuwa ni pamoja na majeraha ya kimwili, matatizo ya afya ya akili, na matatizo ya mahusiano. Kuwa mwadilifu na makini ni sifa za maadili mema hivyo ni njia ya kuepuka vitendo vya kikatili kwa watoto katika jamii. Chati Na. 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swala la 11.




**Chati Na. 11**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 11*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 122,695 (9.05%) waliochagua kipotoshi A, *Kuwa mpole na mnyenyekevu* walipotoka kwani kuwa na unyenyekevu maana yake ni kuwa mtiifu ili kupata kitu. Kwa hiyo hiki si kitendo cha kuepuka vitendo vya kikatili, na kuwa mpole ni kuwa mtulivu; kitendo ambacho hakisaidii kukomesha vitendo vya kikatili. Hivyo, kuwa mpole na mnyenyekevu mbele ya watu wanaoweza kutenda matendo ya kikatili kunaweza kusababisha madhara kwa mtoto, hasa ikiwa mtoto hayuko makini. Watahiniwa katika kundi hili hawakujua kwamba kunyenyekea kunahitajika tu kwa hali nzuri na zinazokubalika na si kwa vitendo visivyo na huruma. Aidha, watahiniwa hao hawakufahamu kuwa kuonesha tabia

ambayo inawaheshimu na kuwajali watu wengine inaweza kuvumiliwa kwa watu wenye nia njema. Vilevile, watahiniwa 72,052 (5.31%) waliochagua kipotoshi C, *Kuwa mpole na mcheshi* hawakuwa sahihi kwa sababu kupendeza, kuvutia na kunyenyekea kwa mtu mwenye nia mbaya kunaweza kusababisha madhara kwa mtoto. Kuwa mcheshi ni kuwa mzungumzaji kwa kuwafanya watu wacheke kupitia maneno au matendo ya mtu; kitendo ambacho hakisaidii kukomesha vitendo vya kikatili. Watahiniwa hao hawakujua kuwa mtoto anahitaji kuonywa na kusema ukweli kwa watu wenye nia mbaya ya vitendo vya kikatili.


Aidha, watahiniwa 65,759 (4.85%) waliochagua kipotoshi D, *Kuwa mchangamfu na mpole* hawakujua kuwa mpole ni hali ya kuonesha tabia nzuri kwa wengine kwa matendo na kwa uungwana. Ni kipengele muhimu katika mwingiliano wa kila siku na watu wengine japokuwa hakiwezi kumlinda mtoto dhidi ya matendo ya kikatili ikiwa tahadhari haiwezi kuchukuliwa. Vivyo hivyo, watahiniwa hawakujua kuwa *uchangamfu* ni hali ya kuwa na furaha, shauku, na hisia chanya. Uchangamfu huleta afya bora, huboresha mahusiano, huongeza ufanisi katika kazi au masomo, hupunguza, msongo wa mawazo, na huongeza nguvu na hamasa. Hata hivyo kuwa mchangamfu hakusaidii kwatoto kuepukana na vitendo vya kikatili vinavyoweza kutokea katika jamii anamoishi.

Vilevile, watahiniwa 31,5079 (23.23%) waliochagua kipotoshi E, *Kuwa mstahimilivu na mwadilifu* hawakujua kwamba ustahimilivu unarejelea uwezo wa mtu binafsi kufanikiwa kukabiliana na hali ngumu au yenye changamoto katika maisha na kuwa na uadilifu ni hali ya kuwa mwaminifu na kuonesha ufuasi thabiti na usiobadilika wa kanuni na maadili. Sifa hizi haziwezi peke yake kumlinda mtoto kutokana na vitendo vya kikatili. Mtoto anapaswa kuchukua hatua za ziada anapotangamana na watu wengine na kuripoti uhalifu kwa mamlaka husika iwapo kuna vitendo vya kikatili. Kwa hivyo, jibu hili lisingeweza kustahili kuwa jibu sahihi.

**Swali la 12:** Ni muhimu kutenda mambo mema kwa wengine kwa namna ambayo wewe ungependa kutendewa. Kitendo kipi kinaonesha kuwajali wengine?

A Kumlisha chakula mgonjwa
B Kuvaa nguo nzuri
C Kusalimia wazee kwa heshima
D Kuvaa nguo za heshima
E Kucheza pamoja na wengine

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini matendo yanayoonesha kuwajali watu wengine katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 703,340 (51.86%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 652,966 (48.14%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kumlisha chakula mgonjwa* waliweza kutofautisha kati ya kujijali mwenyewe na kujali wengine. Kujijali kunahusisha kuchukua hatua za makusudi ili kudumisha na kuboresha mtu kimwili, kihisia, na kiakili kwa mfano kujitunza kimwili, kuburudika na kustarehe. Walielewa kwamba kuwajali wengine kunahusisha kuonesha hisia kwa mwenzi, huruma, na utegemezi kwa watu wa karibu. Mifano ya matendo ya kuwajali wengine ni pamoja na huruma, fadhili, kusikiliza kwa makini na usaidizi. Kujali kuhusu wengine ni muhimu kwa sababu mbalimbali kama vile kuimarishwa kwa mahusiano, ustawi wa kihisia, maelewano ya kijamii, ukuaji wa binafsi, na kuwa mfano mzuri. Chati Na. 12 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 12.




**Chati Na. 12**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 12*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 52,003 (3.83%) waliochagua kipotoshi B, *Kuvaa nguo nzuri* na watahiniwa 67,940 (5.01%) waliochagua kipotoshi D, *Kuvaa nguo za heshima* walishindwa kutofautisha kati ya kujijali na kuwajali wengine. Watahiniwa hao walikosa uelewa kwa kuwa kuweka

mkazo katika mambo binafsi kama vile kuvaa nguo nzuri kuwa nadhifu, kupiga pasi nguo na kuvaa nguo za heshima hudhihirisha kujijali na sio kuwajali wengine.
Aidha, watahiniwa 194,365 (14.33%) waliochagua kipotoshi C, *Kusalimia wazee kwa heshima* hawakuwa sahihi kwa sababu kuwasalimia wazee ni ishara ya heshima ambayo hudhihirika kwa kauli au kitendo cha kirafiki cha mtu mmoja anapokutana na mwingine; huu ni ujumbe wa kutakiana heri. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa kujali ni zaidi ya kuheshimu wazee kwa kuwasalimia.

Vilevile, watahiniwa 323,073 (23.82%) waliochagua kipotoshi E, *Kucheza pamoja na wengine* hawakuwa sahihi kwani kutumia muda pamoja na wengine kushiriki katika jambo la kuburudisha sio lazima lioneshe kuwajali wengine bali kujifurahisha tu.


**Swali la 13**: Amani na usalama katika jamii hujengwa kwa maelewano mazuri. Ni mbinu gani inaweza kutumika kujenga uhusiano mzuri na watu wengine katika jamii?

A Kushirikiana wakati wa raha
B Kushirikishana matatizo ya kifamilia
C Kushirikiana wakati wa shida na raha
D Kuwatembelea ili kujua shida zao
E Kushirikiana wakati wa shida

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* na liliwataka watahiniwa kubainisha mikakati inayotumika kujenga uhusiano mzuri katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306. Watahiniwa 1,084,955 (79.99%) walichagua jibu sahihi na watahiniwa 271,351 (20.01%) hawakujibu swali hili kwa usahihi. Watahiniwa waliobaini jibu sahihi C, *Kushirikiana wakati wa shida na raha* walikuwa na ujuzi kuhusu vipengele hivi. Walijua kwamba nyakati ngumu haziepukiki maishani na zinaweza kujumuisha uzoefu kama vile hasara, ugonjwa, kushindwa, au migogoro. Nyakati hizi zenye changamoto zinaweza kuwa chungu, lakini zinaweza kuwa chanzo cha ukuaji wa binafsi, ustahimilivu, na huruma.

Kwa upande mwingine, nyakati za furaha huchangia hisia ya furaha, na kuridhika zikijumuisha mafanikio, sherehe, uhusiano mzuri na wakati wa raha. Kwa ujumla, nyakati ngumu na za furaha vyote ni vipengele muhimu vya maisha ya binadamu kwani hubadilisha watu, mahusiano, na hata kuathiri jinsi watu wanavyohusiana na kukabiliana na hali mbalimbali. Zaidi

ya hayo, zinachangia ukuaji wa binafsi, kukuza uelewa na huruma, kuimarisha uhusiano wa kijamii, na kuchangia ustawi wa jamii kwa ujumla. Mikakati mingine inayojenga mahusiano mazuri na wengine katika jamii ni pamoja na; kusikiliza kwa bidii, huruma, stadi za mawasiliano, heshima, kusaidiana, uwazi na uaminifu, msamaha, maslahi na shughuli za pamoja. Chati Na 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 13.




**Chati Na. 13***: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 13.*

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa walichagua vipotoshi A, *Kushirikiana wakati wa raha* 45,001 (3.32%) na E, *Kushirikiana wakati wa shida* 76,810 (5.66%). Watahiniwa hawa hawakuweza kung'amua ukweli kwamba uhusiano mzuri haujengwi kwa watu kushirikiana wakati wa raha au shida pekee. Watahiniwa walitakiwa kujua kwamba wanajamii hushirikiana katika hali zote mbaya au nzuri. kwa mfano, kuhudhuria kwenye sherehe za harusi, shughuli za kimichezo, matamasha mbalimbali ya kijamii, misiba pamoja na kusaidia wagonjwa na changamoto nyinginezo. Pia, chaguo B, *Kushirikishana katika matatizo ya kifamilia* lilichaguliwa na watahiniwa 82,563 (6.09%). Watahiniwa hawa hawakutambua kuwa kushirikishana katika matatizo ya kifamilia siyo mbinu pekee ya kujenga uhusiano mzuri. Hii humaanisha njia yenye kuthaminiwa na mjumbe mmojawapo wa familia fulani ili kutafuta kuungwa mkono,


ushauri na ufahamu juu ya jambo fulani nyakati za changamoto ili kurejesha furaha kwa mwanafamilia huyo. Kwahiyo, chaguo hili limejikita kwa mtu mmoja mmoja au ngazi ya familia kuliko jamii nzima.

Zaidi ya hayo, baadhi ya watahiniwa 55,284 (4.08%) walichagua kipotoshi D, *Kuwatembelea ili kujua shida zao*. Watahiniwa hawa walishindwa kujua kwamba kitendo cha kutembelea watu ili kujua shida zao si lazima kihusishe kutatua changamoto zinazowakabili wengine. Kitendo hicho kinaweza kujenga uhusiano mzuri endapo tu kitahusisha msukumo wa dhamira ya kufariji, kushauri, kujali shida za wengine au kutatua changamoto zinazowakabili watu wengine.

**Swali la 14:** Kundi lipi **sio** la watu wenye mahitaji maalumu katika jamii?

A Vijana wenye nguvu
B Watu wenye ulemavu wa kuona
C Watoto wenye ulemavu wa kusikia
D Watu wenye ulemavu wa ngozi
E Watu wenye ulemavu wa akili

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na liliwataka watahiniwa kutambua makundi ya watu wenye mahitaji maalumu katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,168,502 (86.15%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 187,804 (13.85%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Vijana wenye nguvu*, walikuwa wanafahamu kwamba vijana wenye nguvu ni kundi ambalo linaonesha viwango vya juu vya nguvu na utashi. Mara nyingi huwa na shauku, motisha, na kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali. Kwa hivyo, vijana wenye nguvu sio kundi maalumu bali ni kundi la watu wa kawaida. Makundi maalumu ni watu wenye ulemavu ambao unaweza kuhitaji usaidizi wa ziada ili kushiriki katika mambo mbalimbali katika maisha. Kwa mfano ulemavu wa kimwili, hali ya afya ya akili, ulemavu wa ukuaji na mengineyo. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 14.




***Chati Na. 14****: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 14*

Kwa upande mwingine, watahiniwa walioshindwa kubainisha kundi ambalo halikuwa lenye mahitaji maalumu walichagua vipotoshi B, *Watu wenye ulemavu wa kuona* 35,342 (2.61%), C, *Watoto wenye ulemavu wa kusikia 41,352* (3.05%), D, *Watu wenye ulemavu wa ngozi 47,994* (3.54%) na E, *Watu wenye ulemavu wa akili* 52,666 (3.88%). Watahiniwa hawa hawakujua kwamba vipotoshi vyote B, C, D na E vinahusu watu wenye mahitaji maalumu. Watu hawa wana mapungufu ambayo yanaweza kuathiri uwezo wao wa kufanya kazi au shughuli fulani. Kwa mfano, wale waliochagua kipotoshi B, *Watu wenye ulemavu wa kuona* hawakujua kwamba hawa ni watu ambao wamepungua uoni ambao hauwezi kurekebishwa na miwani. Kundi hili linajumuisha vipofu na wenye uoni hafifu na linahitaji usaidizi wa upatikanaji wa zana kama vile fimbo nyeupe.


Aidha, watahiniwa waliochagua kipotoshi C, *Watoto wenye ulemavu wa kusikia,* hawakuelewa watoto wenye ulemavu wa ugumu wa kusikia sauti wanaweza kuwa viziwi. Aina hii inaweza kujumuisha wale walio na usikivu kidogo au uziwi mkubwa. Kadhalika, watahiniwa waliochagua kipotoshi D, *Watu wenye ulemavu wa ngozi* walishindwa kuelewa kuwa kundi hili lenye ulemavu wa ngozi linaweza kusababisha usumbufu mkubwa na kuathiri utendaji kazi wa kila siku. Wengi wa watu hawa wana ngozi ya rangi

iliyopauka, hali hafifu yauoni na ni wanaathirika sana kwa mwanga wa jua. Kwa wale waliochagua kipotoshi E, *Watu wenye ulemavu wa akili*, hawakuwa na uelewa wa kutosha wa kutambua kwamba hawa ni watu wenye ulemavu wa akili na kwamba wanaweza kuwa na matatizo ya utendaji wa utambuzi, ikiwa ni pamoja na kujifunza, mawasiliano, na uamuzi. Mbali na hayo, makundi maalumu yanahitaji ulinzi, upendo, elimu, huduma za afya, na mahitaji muhimu kama chakula, malazi na mavazi.

**Swali la 15**: Ipi ni faida ya matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano kwenye jamii?

A Hutoa takwimu au taarifa sahihi
B Huheshimu usawa wa binadamu
C Husaidia kufanya miamala ya fedha
D Husaidia kutuma ujumbe sahihi
E Husaidia kutunza siri za watu

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uwezo wa watahiniwa kutathmini faida za matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano katika jamii. Swali lilijibiwa na Watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 174,151 (12.84%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,182,155 (87.16%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Husaidia kufanya miamala ya fedha* walikuwa na ufahamu kwamba matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano yanahusisha matumizi bora ya mitandao, salama, na kuwajibika kwa ajili ya kubadilishana taarifa kati ya watu binafsi, vikundi au mashirika. Matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano yanaweza kutoa manufaa makubwa kwa kuboresha miamala; mawasiliano, kuongeza tija, kuimarisha kujifunza; kukuza muunganiko mkubwa na upatikanaji wa habari. Chati Na 15 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 15.





**Chati Na. 15**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 15*

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua vipotoshi A, *Hutoa takwimu au taarifa sahihi watahiniwa* 658,646 (48.56%), B, *Huheshimu usawa wa binadamu* 143,278 (10.56%), D, *Husaidia Kutuma ujumbe sahihi* 258,443 (19.05%) na E, *Husaidia kutunza siri za watu* 109,001 (8.04%) hawakuwa sahihi. Watahiniwa waliochagua vipotoshi hivyo hawakufahamu faida za kutumia mitandao ya mawasiliano ipasavyo. Hivyo, walipaswa kuelewa kwamba hizi ni njia za kuepuka kufanya makosa ya mtandao kama inavyoonesha sheria ya makosa ya Mtandao ya mwaka 2015. Njia nyingine ni pamoja na kusambaza picha zisizo na maadili, kutumia data au taarifa zisizo sahihi, kuepuka kutunga na kutuma habari na ujumbe wa kughushi, kuheshimu usawa wa binadamu wote pamoja na kutunza siri. Kwa hiyo, kwa kuzingatia ufafanuzi huo vipotoshi A, B, D na E havikustahili kuwa majibu sahihi.

**Swali la 16**: Ili nchi iendelee, inahitaji uongozi bora. Sifa ipi inapambanua kiongozi bora katika jamii?

A Kupendwa na watu
B Kuwa mzungumzaji sana
C Kutimiza wajibu
D Kuwa na uwezo wa kifedha
E Kuwa na elimu ya juu

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mwajibikaji* na liliwataka watahiniwa kubaini sifa za kiongozi bora katika jamii. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa1,356,306 ambapo watahiniwa 914,232 (67.41%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 442,074 (32.59%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Kutimiza wajibu* walijua kwamba wajibu ni jambo linalomlazimu mtu kulitimiza; na ambalo hana hiyari nalo katika kulifanya, walijua kuwa kiongozi bora ana maono, huwapa motisha watu anaowaongoza, huwapa matumaini ya kufikia malengo wanayoyatarajia, na huwashirikisha katika kupanga mipango ya kuwaonesha jinsi ya kufanya kazi zao kwa ufanisi ili kuendeleza jamii nzima. Chati Na. 16 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 16.




**Chati Na. 16**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 16*


Kwa upande mwingine, watahiniwa 165,619 (12.21%) waliochagua kipotoshi A, *Kupendwa na watu* hawakuwa sahihi kwa sababu kiongozi bora hafanyi kazi ili kufurahisha au kuridhisha watu kwa mambo yao binafsi bali kiongozi bora hutanguliza maslahi ya jamii mbele. Kwa hiyo, kiongozi bora huchukua hatua stahiki dhidi ya wasiowajibika, hasa wanaokwamisha maendeleo ya jamii kwa ujumla. Vilevile, watahiniwa 51,392 (3.79%) waliochagua kipotoshi B, *Kuwa mzungumzaji sana*, walikosea kwa sababu kupenda kuongea sana au kupiga soga mahali pa kazi sio sifa ya watu wanaowajibika. Aidha, watahiniwa 40,565 (2.99%) waliochagua kipotoshi

D, *Kuwa na uwezo wa kifedha* na 174,583 (12.87%) waliochagua kipotoshi E, *Kuwa na elimu ya juu* nao hawakuwa sahihi kwa sababu hali ya kiuchumi na kiwango cha elimu sio vigezo vya msingi kumfanya mtu awe kiongozi bora. Kwa mfano, kuna viongozi ambao ni wabinafsi na wala rushwa japokuwa wana uwezo wa kiuchumi. Vilevile, kuna watu wenye elimu ya juu lakini wanatoa maamuzi mabaya. Mtu aliyesoma ana sifa ya kuwa mbunifu, mwaminifu na mwenye kupanga malengo na kuyatekeleza. Hivyo kiwango cha juu cha elimu peke yake hakimfanyi mtu kuwa kiongozi bora.

**Swali la 17**: Muda ni miongoni mwa rasilimali zinazochangia katika maendeleo endelevu. Je, nini kinahitajika ili kutumia muda vizuri?

A Kupangilia matukio kulingana na fursa
B Kupangilia mambo yajayo kwa kuangalia rasilimali
C Kupangilia majukumu kulingana na rasilimali
D Kupangilia mambo yajayo kwa kuzingatia fedha
E Kupangilia matukio kulingana na vipaumbele

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na liliwataka watahiniwa kubainisha vigezo vya kutumia vema rasilimali zilizopo kwa maendeleo endelevu yakiwemo matumizi ya muda. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 179,185 (13.21%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 1,177,121 (86.79%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi E, *Kupangilia matukio kulingana na vipaumbele* walijua kuwa kupangilia muda vizuri kunahusisha mchakato wa kuandaa na kupanga jinsi ya kutenga muda kwa shughuli maalumu. Hili linahusisha kuweka malengo, vipaumbele vya kazi, na kupanga wakati kwa njia ifaayo ili mtu atumie wakati huo vizuri. Kupanga matukio kulingana na vipaumbele kuna faida nyingi kama vile: kuboresha mtazamo, kuongeza ufanisi, kuongeza uzalishaji, kupunguza msongo wa mawazo, na kufanya maamuzi bora. Kiuhalisia, kutumia vizuri muda kunahitaji vipengele kadhaa muhimu kama vile kuweka malengo, kuweka kipaumbele kwa kazi, kugawa majukumu katika hatua ndogo ndogo na kuweka ukomo. Chati Na. 17 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 17.





**Chati Na. 17**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 17*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 290,501 (21.42%) waliochagua kipotoshi A, *Kupangilia matukio kwa kulingana na fursa* hawakuwa sahihi kwa sababu dhana hiyo inahusu tendo la kupanga matukio kwa kuzingatia tukio au hali inayofanya uwezekano wa tukio hilo kufanyika, na si kwa nia ya kuokoa muda. Vilevile, watahiniwa 188,037 (13.86%) waliochagua kipotoshi B, *Kupangilia mambo yajayo kwa kuangalia rasilimali,* 617,719 (45.54%) waliochagua kipotoshi C, *Kupangilia majukumu kulingana na rasilimali* na watahiniwa 64,347 (4.74%) waliochagua kipotoshi D, *Kupangilia mambo yajayo kwa kuzingatia fedha* hawakuwa sahihi pia kwa sababu vipotoshi vyote vinatilia mkazo kupanga kwa kuzingatia rasilimali. Rasilimali hizo ni kama vile rasilimali za asili, fedha na rasilimali watu ambazo zinaweza kuwezesha kukamilika kwa matukio, jambo ambalo ni kinyume na matumizi mazuri ya muda.

**Swali la 18**: Rasilimali za shule zinaweza kutumika kuleta maendeleo, na ni wajibu wa kila mmoja kuzilinda. Hatua zipi zinatakiwa kuchukuliwa katika kufanya utunzaji wa rasilimali hizo?

A Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara
B Kufanya ukaguzi na kutoa taarifa
C Kufanya ukaguzi na kuzigawa rasilimali kwa watu
D Kufanya ukaguzi na kununua rasilimali mpya
E Kufanya ukaguzi na kuzitupa

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mwajibikaji na* lilipima uwezo wa watahiniwa wa kubaini mikakati inayoweza kusaidia kutunza rasilimali za shule. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 585,535 (43.17%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 770,771 (56.83%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Kufanya ukaguzi na kutoa taarifa*, walikuwa na uelewa kwamba rasilimali za shule ni pamoja na nyenzo, mali, na huduma mbalimbali ambazo shule inazihitaji ili kufanya kazi kwa ufanisi na kutoa elimu bora. Rasilimali hizi zinaweza kuwa halisi kama majengo, madarasa, vifaa vya michezo, vya maabara, teknolojia (kompyuta, projekta) na mali nyingine zinazoonekana (samani, vitabu, vifaa vya kufundishia). Rasilimali hizi ni muhimu kwa utendaji mzuri na mafanikio ya shule. Baadhi ya hatua ambazo shule zinaweza kuchukua ili kuzidhibiti ni pamoja na matengenezo, utunzaji, ufuatiliaji na tathmini na usimamizi wa idadi ya vifaa. Hatua hizo zinajumuisha kujenga utamaduni wa kuzuia uharibifu na matengenezo ili kutoa ufanisi wa kutoa elimu bora zaidi kwa wanafunzi. Chati Na. 18 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 18.





**Chati Na. 18**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 18*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 525,837 (38.77%) waliochagua kipotoshi A, *Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara* hawakuwa sahihi kwa sababu ukaguzi bila kuandika taarifa haisaidii uongozi wa shule kujua uchakavu au uharibifu uliobainika wakati wa ukaguzi ili kufanya matengenezo kwa muda unaotakiwa. Vivyo hivyo, kwa watahiniwa 97,011 (7.15%) waliochagua kipotoshi C, *Kufanya ukaguzi na kuzigawa rasilimali kwa watu* na 51,362 (3.79%) waliochagua kipotoshi E, *Kufanya ukaguzi na kuzitupa* hawakuwa sahihi kwa sababu vipotoshi vyote viwili vilibeba matendo ambayo yanatumia vibaya rasilimali za shule. Matumizi mengine mabaya ya rasilimali za shule ni pamoja na matumizi ya mali ya shule kwa faida binafsi, kutupa rasilimali, na matumizi mabaya ya fedha za shule. Mwisho, watahiniwa 83,521 (6.16%) waliochagua kipotoshi D, *Kufanya ukaguzi na kununua rasilimali mpya*, hawakujua kwamba kununua rasilimali mpya sio mbinu ya kulinda zilizopo zisiharibike. Kwa mantiki hiyo, uwepo wa taarifa baada ya ukaguzi husaidia uongozi wa shule kufanya maamuzi sahihi juu ya rasilimali kama zinahitaji kukarabati, kuuzwa au kununuliwa mpya.

**Swali la 19**: Matendo yafuatayo hujenga nidhamu binafsi kwa wanafunzi **isipokuwa:**

A kumaliza kazi kwa wakati.
B kuwa na ratiba ya kujisomea.
C kusoma kwa bidi.
D kutumia muda vizuri.
E kusuburi kupangiwa majukumu.

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini matendo yanayojenga nidhamu binafsi kwa wanafunzi. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,071,945 (79.03%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 284,361 (20.97%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi E, *kusubiri kupangiwa majukumu* walielewa kuwa nidhamu binafsi ni uwezo wa kujitawala na kufanya maamuzi kwa kuzingatia akili badala ya msukumo. Watahiniwa walielewa sifa za mtu mwenye nidhamu binafsi kuwa ni pamoja na kutumia muda vizuri, uthabiti, nia thabiti, uwajibikaji, kubadilika kulinga na hali halisi, mwelekeo wa malengo, ustahimilivu, uvumilivu, kujidhibiti na uwajibikaji. Chati Na. 19 inaonesha ufaulu katika swali la 19.




**Chati Na. 19**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 19*

Hata hivyo, watahiniwa 76,037 (5.61%) waliochagua kipotoshi A, *kumaliza kazi kwa wakati* walishindwa kutofautisha tendo lisilo sahihi katika kujenga nidhamu binafsi kwa wanafunzi. Kumaliza kazi kwa wakati ni sifa mojawapo ya kuwa na nidhamu binafsi kwani hakuna jitihada nyingine iliyofanyika kuhakikisha kuwa kazi inakamilika kwa wakati uliowekwa. Vilevile, watahiniwa 64,258 (4.74%) waliochagua kipotoshi B, kuwa *na ratiba ya kujisomea* hawakuwa sahihi kwa sababu kuwa na mtirirIko unaoonesha shughuli mbalimbali za kitaaluma na muda maalumu kwa kila shughuli ni kitendo kinachoashiria nidhamu binafsi. Nidhamu binafsi, humfanya mwanafunzi kujua ni shughuli gani aifanye na ni kwa muda gani.


Aidha, watahiniwa 80,426 (5.93%) waliochagua kipotoshi C, *kusoma kwa bidii* hawakuwa sahihi kwani kusoma kwa bidii huhusisha kutumia muda na umakini wa hali ya juu katika kujipatia maarifa ya masuala ya kitaaluma. Watahiniwa hawa walikosa uelewa kuwa kusoma kwa bidii huhitajika sana ili kufanikisha upatikanaji wa maarifa na ujuzi, na hii ni sifa au kigezo kimojawapo cha nidhamu binafsi. Pia, watahiniwa 50,698 (3.74%) waliochagua kipotoshi D, *kutumia muda vizuri* hawakuwa sahihi kwa sababu mchakato wa kupanga na kutumia muda vizuri kwenye shughuli maalumu unahitaji nidhamu binafsi. Nidhamu binafsi kimsingi ni takwa la kimsingi ambalo lina umuhimu mkubwa katika maendeleo ya kielimu na ya kibinafsi kwa wanafunzi. Nidhamu inawawezesha kufikia malengo yao, kutumia muda wao kwa ufanisi, kudhibiti hisia zao na kuendeleza tabia nzuri inayochangia ustawi wao kwa ujumla na mafanikio katika maisha.

**Swali la 20**: Rushwa imekuwa kikwazo kikubwa katika maendeleo ya nchi. Ni njia ipi kati ya hizi zifuatazo **sio** ya kuzuia na kupambana na rushwa nchini?

| | | |
|---|---|---|
| A Uwazi | B Uzalendo | C Uadilifu |
| D Ustahimilivu | E Uwajibikaji | |

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini njia mbalimbali za kuzuia na kupambana na rushwa nchini. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 610,426 (45.01%) walijibu swali hili kwa usahihi na Watahiniwa 745,880 (54.99%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Ustahimilivu* walitambua kuwa ustahimilivu unahusu uwezo wa kukabiliana na ugumu au changamoto. Inahusisha

kunyumbulika, na kuweza kudumisha mtazamo unaofaa wakati wa matatizo. Watahiniwa hawa walielewa kuwa ustahimilivu si njia ya moja kwa moja ya kuzuia na kupambana na rushwa bali huwapa watu uwezo wa kukabiliana na changamoto zinazowakabili maishani kwa kuwajengea ujasiri, matumaini na uwezo wa kustahimili hali ngumu. Chati Na. 20 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 20.




***Chati Na. 20****: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 20*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 166,626 (12.29) waliochagua kipotoshi A, *Uwazi*, watahiniwa 219,742 (16.20%) waliochagua kipotoshi B, *Uzalendo*, watahiniwa 172,879 (12.75%) waliochagua C, *Uadilifu* na watahiniwa 170,245 (12.55%) waliochagua kipotoshi E, *Uwajibikaji*, hawakutambua kwamba vipotoshi A, B, C na E vilikuwa ni njia sahihi za kuzuia na kupambana na rushwa. Kwa mfano, watahiniwa waliochagua kipotoshi A, *Uwazi* hawakujua kwamba hii inarejelea hali ya kuwa mwaminifu, bayana katika matendo, maamuzi, na mawasiliano baina ya mtu na mtu. Inahusu kutoa ufikishaji wa habari na kufanya michakato ionekane kwa wengine. Hivyo, inasaidia kupambana na rushwa. Uwazi huruhusu ugunduzi na kupunguza uwezekano wa tabia ya rushwa.

Pia, watahiniwa waliochagua kipotoshi B, *Uzalendo,* hawakutambua kuwa uzalendo unahusisha upendo na kujitolea kwa mtu kwa nchi yake. Mara nyingi huhusisha hisia ya ufahari kwa taifa lake na hamu ya kuchangia


ustawi wake. Kadhalika, uzalendo unakuza hali ya uaminifu, wajibu wa kiraia, fahari ya kitaifa na msaada kwa nchi yako. Kwa hiyo, uzalendo unasaidia katika vita dhidi ya vitendo vya rushwa kutoka moyoni. Vilevile, watahiniwa waliochagua kipotoshi C, *Uadilifu,* hawakutambua kuwa ni hali ya kuwa mwaminifu na kuwa na maadili mema. Msingi unaotokana na maadili kama vile uaminifu, uadilifu na kanuni thabiti za maadili. Inahusisha kufanya jambo sahihi, hata kama hakuna anayelitazama, hivyo kuwa moja ya nyenzo zinazosaidia kupambana na rushwa katika jamii.

Vivyo hivyo, watahiniwa wengine waliochagua kipotoshi E, *Uwajibikaji* hawakuelewa kuwa ni ulazima wa kuwajibika kwa mtu kutokana na matendo yake, maamuzi, na matokeo yanayotokana nayo. Inahusisha kuwa muwazi, mwaminifu na kuwa tayari kuwajibika kwa matendo yako. Kwa hiyo, kila mwananchi anayewajibika ana wajibu wa kijamii kushiriki katika vita dhidi ya vitendo vya rushwa nchini.

**Swali la 21**: Tendo lipi linaonesha uwepo wa utawala bora katika ngazi ya familia?

A Kununulia familia nguo nzuri na za kisasa
B Kuhakikisha kuwa wanafamilia wote wanapata haki sawa
C Uwepo wa chakula kitamu kwa wanafamilia
D Uwepo wa samani nzuri na za gharama nyumbani
E Watoto kuwa huru kuchagua marafiki zao

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuheshimu Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini matendo yanayoonesha uwepo wa utawala bora katika ngazi ya familia. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,135,582 (83.73%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 220,724 (16.27%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Kuhakikisha kuwa wanafamilia wote wanapata haki sawa* walikuwa wanafahamu utawala bora katika ngazi ya familia, ikimaanisha mawasiliano yenye ufanisi, ushirikiano, na usimamizi wa rasilimali ili kusaidia ustawi wa wanafamilia wote. Baadhi ya viashiria vya utawala bora katika ngazi ya familia ni pamoja na michakato ya maamuzi ya mawasiliano ya wazi na yenye ufanisi, utatuzi wa migogoro, usimamizi wa fedha, majukumu ya pamoja, msaada na matunzo, heshima kwa wote na uwajibikaji wa kijamii. Chati Na. 21 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 21.




**Chati Na. 21**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 21*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 56,441 (4.16%) waliochagua kipotoshi A, *Kununulia familia nguo nzuri na za kisasa* na watahiniwa 45,838 (3.38%) waliochagua kipotoshi D, *Uwepo wa samani nzuri na za gharama nyumbani* walishindwa kutambua kuwa haki sawa kwa wanafamilia wote ni muhimu zaidi kuliko kuvaa nguo nzuri na za kisasa.


Vilevile, watahiniwa, 53,405 (3.94%) waliochagua kipotoshi C, *Uwepo wa chakula kitamu kwa wanafamilia* hawakuwa sahihi kwasababu chakula chenye ladha nzuri na cha kupendeza sio kigezo pekee cha uwepo wa utawala bora katika ngazi ya familia. Aidha, watahiniwa 54,797 (4.04%) waliochagua kipotoshi E, *Watoto kuwa huru kuchagua marafiki* hawakuwa sahihi kwa kuwa uhuru wa watoto una mipaka; wazazi au walezi wanapaswa kuwaongoza watoto wao kuchagua marafiki wenye mienendo mizuri. Pia, watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa baadhi ya watoto wanaweza kuwa na tabia mbaya kama wakiachwa huru kuchagua marafiki wanaowataka.

**Swali la 22:** Kijiji cha Mtama hakina vyanzo vya maji kwa sababu ya uharibifu wa mazingira uliosababishwa na ukataji miti kupita kiasi. Je, jamii inapaswa kufanya nini ili kuboresha mazingira yake?

A Kupanda miti mingi katika eneo husika
B Kutengeneza bustani katika eneo husika
C Kuanzisha miradi ya kilimo cha umwagiliaji
D Kuanzisha mradi wa kuuza miti
E Kutumia walinzi wa kulinda mazingira

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuithamini Jamii* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini njia za kutatua uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,081,149 (79.71%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 275,157 (20.29%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kupanda miti mingi katika eneo husika* walielewa sababu kuu za kupanda miti katika eneo kuwa ni uboreshaji wa hewa, kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa, udhibiti wa mmomonyoko wa udongo, uhifadhi wa maji, uhifadhi wa viumbe hai, udhibiti wa mabadiliko ya tabia nchi na kuleta faida za kiuchumi.

Kadhalika, walielewa kuwa uharibifu wa mazingira unasababisha athari kadhaa kama vile ongezeko la joto duniani, kupoteza viumbe hai, kupoteza unyevu wa udongo, jangwa na mmomonyoko wa udongo. Aidha, watahiniwa hao walijua njia mbalimbali za kuboresha mazingira kama vile upandaji miti na upandaji miti upya, urejeshaji wa makazi, kuzuia uchafuzi wa mazingira, kudhibiti mmomonyoko wa ardhi, ushirikishwaji wa jamii na elimu, na usimamizi endelevu wa rasilimali. Chati Na. 22 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 22.




**Chati Na. 22**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 22*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 48,783 (3.60%) waliochagua kipotoshi B, *Kutengeneza bustani katika eneo husika* hawakuwa sahihi kwa sababu uwepo na muendelezo wa bustani huhitaji uwepo wa maji muda wote na kama eneo husika lina uhaba wa maji ni vigumu kuendeleza bustani. Vilevile, watahiniwa 78,015 (5.75%) waliochagua kipotoshi C, *Kuanzisha miradi ya kilimo cha umwagiliaji* hawakujua kuwa, mbinu zinazotumika katika skimu za umwagiliaji kama vile kushuka kwa maji mvuto au mfumo wa mifereji ya maji ya pampu, uvunaji wa maji na mifumo ya mgandamizo ya maji kama vile matone na vinyunyiziaji; inahitaji uwepo wa maji kwa muda wote.

Aidha, watahiniwa 50,462 (3.72%) waliochagua kipotoshi D, *Kuanzisha mradi wa kuuza miti* hawakuwa sahihi kwa sababu, mradi wa kuuza miti huchochea tatizo la ukosefu wa maji kuliko kulitatua. Hii ni kutokana na ukweli kwamba uwepo wa miti husaidia kuhifadhi vyanzo vya maji ambapo maji hutiririka kutokea huko kuelekea kwenye mito, na pia miti husaidia kuleta mvua kwa njia ya mvuke kutoka kwenye mimea. Vilevile, watahiniwa 86,978 (6.41%) waliochagua kipotoshi E, *Kutumia walinzi wa kulinda mazingira* walishindwa kujua vyanzo vikuu vya uharibifu wa mazingira na hatua stahiki zinazochukuliwa ili kupambana na changamoto hiyo. Uwepo wa walinzi kwenye eneo ambalo limeishaharibiwa kutokana na ukataji miti

uliokithiri hakuna tija wala suluhisho lolote. Kutumia walinzi haiwezi kuwa njia sahihi kwa kuwa wananchi wote wanatakiwa kushiriki katika kutunza mazingira.

**Swali la 23**: Seti ipi kati ya zifuatazo inawakilisha kwa usahihi kanuni za kuzingatiwa kwenye ushirikiano wa wanafunzi shuleni?

A Kuheshimiana, kufanya kazi kwa bidii, kushauriana na kuwa waadilifu

B Kufanya kazi kwa bidii, kuheshimiana, kufichua maovu na kuwa wakweli


C Heshima, ufanisi, ushauri, ustahimilivu na uadilifu

D Kufanya kazi kwa bidii, uvumilivu, unasihi na kupuuza wengine

E Uwajibikaji, uvumilivu, kujitambua na kujiamini

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu kanuni za kuzingatiwa kwenye ushirikiano wa wanafunzi shuleni. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 303,500 (22.38%) walijibu kwa usahihi ikilinganisha na watahiniwa 1,052,806 (77.62%) walioshindwa kujibu kwa usahihi. Waliochagua jibu sahihi B, *Kufanya kazi kwa bidii, kuheshimiana, kufichua maovu na kuwa wakweli* walikuwa wanafahamu maelezo ya kujenga mazingira chanya na yenye tija ya kujifunzia. Kanuni hiyo inajumuisha kukuza mpangilio unaohimiza kujifunza, kujihusisha, na ukuaji wa kibinafsi. Hii inahusisha kujenga mazingira ambapo wanafunzi wanahisi kuwa salama, kuungwa mkono, na kuhamasishwa kuchukua tahadhari na changamoto zao. Inamaanisha pia kutoa nyenzo, zana, na usaidizi unaohitajika kwa wanafunzi kufaulu kitaaluma. Baadhi ya njia zinazoweza kuhimiza na kuwezesha ushirikiano miongoni mwa wanafunzi ni pamoja na majadiliano ya darasani, kazi za vikundi; na kuhimiza ujumuishi.

Vile vile, ushirikiano una umuhimu mkubwa kwa wanafunzi shuleni kwa sababu mbalimbali kama vile maendeleo ya kijamii, mafanikio ya kitaaluma, kutatua matatizo shuleni, ustawi wa kihisia, mawasiliano yaliyoimarishwa, stadi za uongozi na kuboresha mazingira ya kujifunzia. Chati Na 23 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 23.




***Chati Na. 23**: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 23*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 671,593 (49.52%) waliochagua kipotoshi A, *Kuheshimiana, kufanya kazi kwa bidii, kushauriana na kuwa waadilifu* hawakutambua kuwa chaguo hili lilijumuisha dhana ya *Kuwa mwadilifu* ambayo kimsingi humanisha sifa ya kuwa mwaminifu, mkweli na kufuata misingi thabiti ya maadili ya jamii. Uadilifu siyo tu kanuni ya ushirikiano bali ni sifa ya kibinadamu inayosaidia kupambana na rushwa kwa sababu imejikita katika kufuata maadili ya jamii. Vivyo hivyo, watahiniwa 150,208 (11.07%) waliochagua C, *Heshima, ufanisi, ushauri, ustahimilivu na uadilifu* hawakuelewa kuwa istilahi hizi hazikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na misingi inayotakiwa kuzingatiwa kwenye ushirikiano wa wanafunzi shuleni. Kwa mfano, ufanisi huelezea madhumuni ya kutathmini utendaji wa shughuli fulani.

Aidha, ustahimilivu unahusisha njia mbalimbali za kukabiliana na changamoto za kila siku. Inamaanisha uwezo wa kustahimili kurudi katika hali ya kawaida kutoka kwenye hali ngumu anayokabiliana nayo kufanya jambo bila kupoteza muda, nyenzo au nguvu ili kazi iliyofanywa iwe ya haraka na haina makosa. Humpa mtu ujuzi unaohitajika ili kumwezesha kutumia wakati, akili na nguvu ya kihisia ili kupata ufumbuzi wa matatizo yanayomkabili.

Zaidi ya hayo, watahiniwa 52,637 (3.88%) walichagua kipotoshi D, *Kufanya kazi kwa bidii, uvumilivu, unasihi na kupuuza wengine*. Hao pia hawakuzingatia ukweli kuwa chaguo D lilijumuisha majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, dhana ya *kupuuza wengine* humaanisha kitendo cha makusudi cha kutojali maoni, hisia na changamoto za watu wengine. Tabia ya kutowajali wengine hujenga sifa ya ubinafsi, kujisifu na kiburi. Kiuhalisia, inapingana na misingi ya kujenga uhusiano mzuri shuleni.


Sambamba na hilo, watahiniwa 163,426 (12.05%) waliochagua kipotoshi E, *Uwajibikaji, uvumilivu, kujitambua na kujiamini,* walishindwa kutambua misingi isiyofaa kuzingatiwa kwenye ushirikiano kuwa ni pamoja na kujitambua na kujiamini. Istilahi hizi zilihusiana na ujuzi wa maisha ya mtu binafsi ambapo kujitambua ni hali ya mtu kijielewa kiyakinifu ikiwa ni pamoja na kuelewa hisia, tabia, uimara na udhaifu wake. Vivyo hivyo, *kujiamini* ni hulka ya kuwa na mtazamo chanya juu yako mwenyewe kwa kuamini katika uwezo, ujuzi alionao na uwezo wa kuendesha maisha yako. Hivyo, dhana hizo tajwa hazikustahili kuwa jibu sahihi.

**Swali la 24**: Iwapo utachaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza mwaka 2024, ni njia zipi utazitumia kupata maarifa na taarifa mbalimbali?

A Kusoma vitabu na matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano
B Kutumia mtandao ya mawasiliano na kusikiliza muziki
C Kusikiliza muziki, kuangalia taarifa ya habari na kusoma vitabu
D Kuangalia taarifa ya habari, kutembelea marafiki na kusikiliza radio
E Kusikiliza radio, kutembelea marafiki na kusoma vitabu

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mstahimilivu* na liliwataka watahiniwa kubainisha njia sahihi zinazotumika kupata maarifa na taarifa katika mchakato wa kujifunza shuleni. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306, ambapo watahiniwa 813,065 (59.95%) walilijibu kwa usahihi na watahiniwa 543,241 (40.05%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kusoma vitabu na matumizi sahihi ya mitandao ya mawasiliano*, walifahamu vyanzo vya maarifa na taarifa za kitaalamu.

Aidha, walikuwa wanafahamu kwamba mitandao ya mawasiliano inaweza kutoa taarifa muhimu za kitaaluma na maarifa kwa njia ya intaneti, kujifunza kwa masafa na elimu ya mtandaoni, upatikanaji wa taarifa nyingi, utafiti kujisomea na kujifunza maisha. Kwa mfano, uwepo wa mtandao umekuwa nyenzo kuu ya kujifunza kwa ufanisi kwani imerahisisha wanafunzi kutafuta makala, habari, video za mafunzo, makala na maudhui mengine ya kujifunza. Kwa kifupi, watahiniwa hawa walifahamu kuwa mitandao ya mawasiliano ni chanzo muhimu cha taarifa iwapo itatumiwa ipasavyo. Chati Na. 24 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 24.




**Chati Na. 24** : *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 24*


Hata hivyo, watahiniwa 62,182 (4.58%) waliochagua kipotoshi B, *Kutumia mtandao ya mawasiliano na kusikiliza muziki* na watahiniwa 79,843 (5.89%) waliochagua kipotoshi C, *Kusikiliza muziki, kuangalia taarifa ya habari na kusoma vitabu* hawakuelewa kuwa kusikiliza muziki sio chanzo kikuu cha habari ya kuelimisha kwani yaliyomo katika muziki hayajapangwa kwa njia ya kutumika katika masomo fulani katika mtaala wa shule. Badala yake muziki unaweza kuwasaidia wanafunzi kupumzika, kujiburudisha, kuhisi motisha, na kuboresha kumbukumbu.

Kadhalika, watahiniwa 204,218 (15.06%) waliochagua kipotoshi D, *Kuangalia taarifa ya habari, kutembelea marafiki na kusikiliza radio* na watahiniwa 182,607 (13.46%) waliochagua kipotoshi E, *Kusikiliza radio, kutembelea marafiki na kusoma vitabu* hawakuelewa kuwa lengo la kutembelea marafiki ni kuwaonesha upendo na sio kupata maarifa na taarifa. Pia, kuna marafiki ambao hujiunga kwenye makundi mabaya, kwa hiyo hawafai kuwa chanzo cha maarifa. Kwa ujumla vichaguzi hivyo havikuweza kukidhi matakwa ya majibu sahihi.

**Swali la 25**: Wanafunzi wana wajibu wa kujifunza kwa vitendo wanapokuwa nyumbani. Ni shughuli zipi wanaweza kujifunza wakiwa nyumbani?

A Kufua nguo na kuosha vyombo
B Kuosha vyombo na kusafisha darasa
C Kufua nguo na kufuta ubao
D Kufagia darasa na kulisha mifugo
E Kulisha mifugo na kufagia ofisi

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mwajibikaji* na liliwataka watahiniwa kubaini shughuli ambazo mwanafunzi anaweza kujifunza akiwa nyumbani. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,188,820 (87.65%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 167,486 (12.35%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kufua na kuosha vyombo* walifahamu kuwa wanafunzi hujifunza kuwa na nidhamu binafsi, kuwajibika na kufanya kazi hata wanapokuwa nje ya shule. Pia, walijua kuwa shughuli hizi zinaweza kukamilisha elimu yao rasmi ya darasani na kuwasaidia kupata stadi muhimu za maisha. Baadhi ya mifano ya shughuli hizo ni ujuzi wa kilimo, stadi za kusoma na kuandika, ufahamu wa mazingira, stadi za maisha, afya na usafi, sanaa na ufundi, maarifa ya kitamaduni na historia, ujasiriamali na stadi za biashara, elimu ya mazingira na elimu ya viungo na michezo na huduma za jamii na kujitolea. Kwa kushiriki katika shughuli hizi, wanafunzi wanaweza kuchangia maendeleo yao binafsi, familia zao na jumuiya zao. Wanaweza pia kuwa na jukumu la kuhifadhi na kuendeleza tamaduni na mila za Kitanzania, wakati huo huo wakijitayarisha kwa mustakabali mwema wa maisha yao. Chati Na. 25 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 25.





**Chati Na. 25**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 25*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 50,925 (3.75%) waliochagua kipotoshi B, *Kuosha vyombo na kusafisha darasa*, watahiniwa 39,444 (2.91%) waliochagua kipotoshi C, *Kufua nguo na kufuta ubao*, watahiniwa 34,084 (2.51%) waliochagua kipotoshi D, *Kufagia darasa na kulisha mifugo* na watahiniwa 33,418 (2.46%) waliochagua kipotoshi E, *Kulisha mifugo na kufagia ofisi* hawakuwa sahihi kwa sababu vipotoshi hivi vilijumuisha majukumu ambayo siyo ya nyumbani. Mathalani, kufagia au kusafisha madarasa, ofisi na ubao ni kazi ambazo mwanafunzi huzifanya akiwa shuleni na sio nyumbani. Kadhalika, shule hufundisha shughuli kadhaa zikiwemo elimu ya viungo na michezo, elimu ya kilimo na mazingira, ujuzi wa ujasiriamali, sanaa ya kitamaduni na jadi, elimu ya kifedha, na ya uraia, mijadala na kuzungumza na kuzungumza mbele ya hadhara na huduma za kijamii pamoja na za kujitolea.

**Swali la 26**: Wanafunzi wanatakiwa kuwa wadadisi katika mchakato wa kujifunza. Ni njia ipi wanapaswa kutumia ili wawe wadadisi?

A Kuuliza maswali na kujisomea
B Kujisomea na kuiga kwa wanafunzi wenye akili
C Kusoma vitabu na kucheza michezo mingi
D Kutumia mitandao ya kijamii muda wote
E Kufanya majaribio na kucheza michezo mbalimbali

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mstahimilivu* na lilitaka watahiniwa kubaini njia zinazotumika wakati wa ufundishaji kwa njia ya udadisi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,076,434 (79.37%) walilijibu kwa usahihi na watahiniwa 279,872 (20.63%) hawakulijibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kuuliza maswali na kujisomea* walikuwa na ujuzi juu ya mchakato wa kujifunza kwa kudadisi. Walijua kwamba mbinu hiyo inawahimiza wanafunzi kuuliza maswali, kutafuta majibu, kujihusisha kikamilifu na somo, kukuza udadisi, kufikiri kwa kina na ujuzi wa kutatua matatizo. Baadhi ya mbinu za kujifunza kwa udadisi ni pamoja na kujifunza kwa msingi wa uchunguzi, ujifunzaji unaotegemea matatizo, ujifunzaji unaotegemea mradi, na ujifunzaji unaozingatia kesi na ujifunzaji shirikishi. Kwa ujumla, kuuliza maswali na kujisomea kunasaidia katika kujifunza kwa sababu husisitiza udadisi wa wanafunzi, kuuliza maswali na kufanya uchunguzi ili kujenga maarifa. Chati Na. 26 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 26.




**Chati Na. 26**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 26*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 99,316 (7.32%) waliochagua kipotoshi B, *Kujisomea na kuiga kwa wanafunzi wenye akili*, watahiniwa 45,420 (3.35%) waliochagua kipotoshi C, *Kusoma vitabu na kucheza michezo mingi* na watahiniwa 74,077 (5.46%) waliochagua kipotoshi E, *Kufanya majaribio na kucheza michezo mbalimbali* hawakuwa sahihi kwa sababu vipotoshi hivi vilihusisha shughuli ambazo sio za kujifunza kwa udadisi. Kwa mfano, wakati mwanafunzi anaiga kutoka kwa wanafunzi wenye akili anaweza kukuza utegemezi wa kujifunza. Zaidi ya hayo, kama wanafunzi wanaiga, uwezo wao wa kujifunza hautakuwa mkubwa zaidi kuliko wanafunzi ambao wanaiga kutoka kwao kwa sababu kuiga kunapunguza utu wao wa ndani, kunayafanya maendeleo yao ya kiakili kudumazwa.

Aidha, kucheza michezo shuleni huwatia moyo wanafunzi kujifunza, huwafanya wawe makini, wakuze fikra zao za kina, washiriki shughuli za darasani na kujiburudisha wanapochoka. Hata hivyo, matumizi kupita kiasi ya michezo katika elimu hayawafanyi wanafunzi kuwa wadadisi kwani husababisha athari hasi kama vile uraibu na masuala ya afya ya akili kama vile mfadhaiko, wasiwasi wa kijamii, ukosefu wa motisha, udhibiti mbaya wa kihisia, usingizi duni na ukosefu wa kufikiria kwa makini. Hatimaye, hii inaweza kuathiri utendaji wa jumla na maendeleo ya wanafunzi.


Vilevile, watahiniwa 50,906 (3.75%) waliochagua kipotoshi D, *Kutumia mitandao ya kijamii muda wote* hawakuwa sahihi kwa sababu wanafunzi wanaotumia muda mwingi kwenye mitandao ya kijamii wanakuwa waraibu na wanaweza kuteseka kutokana na usingizi duni, uchovu wa macho na wanaweza kupata taarifa za uongo, mfadhaiko na wasiwasi.

**Swali la 27** : Utakapoanza masomo ya sekondari Kidato cha Kwanza mwaka 2024, ni aina ipi ya wanafunzi unapaswa kushirikiana nao unapokuwa shuleni ?

A Wenye utiifu kwa viongozi wa shule
B Wenye ujuzi wa kucheza michezo mbalimbali
C Wasomaji wa vitabu vingi
D Wenye nidhamu nzuri
E Wenye kujiamini wakati wote

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mstahimilivu* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini aina ya watu wanaotakiwa kushirikiana nao wakati wa kujifunza shuleni. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306,

ambapo watahiniwa 997,734 (73.56%) walilijibu kwa usahihi na watahiniwa 358,572 (26.44%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Wenye nidhamu nzuri* walikuwa wanafahamu kuwa wanafunzi wenye nidhamu ni watu ambao mara kwa mara wanafuata sheria, miongozo, na matarajio yaliyowekwa na walimu, wazazi au viongozi wengine wenye mamlaka. Mara nyingi huonesha sifa fulani zinazowatofautisha na wasio na nidhamu. Wanafunzi wenye nidhamu wana sifa zifuatazo: kutunza muda/wakati, uwajibikaji, heshima, kujidhibiti, motisha, utunzaji wa wakati, umakini, uadilifu, kuwa na mtazamo chanya na malengo/maono. Sifa hizo humsaidia mwanafunzi kufaulu kitaaluma na kuchangia ukuaji na maendeleo yao binafsi kwa ujumla. Chati Na. 27 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 27.




**Chati Na. 27**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 27*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 95,820 (7.06%) waliochagua kipotoshi A, *Wenye utiifu kwa viongozi wa shule* hawakujua kwamba kuwa na heshima ni sifa ya mtu mwenye nidhamu; kwa maana kwamba nidhamu ya mwanafunzi hudhihirishwa kwa kukubali na kutii amri halali, sheria na kuonesha unyenyekevu kwa mamlaka ya shule. Aidha, watahiniwa 56,631 (4.18%) waliochagua kipotoshi B, *Wenye ujuzi wa kucheza michezo mbalimbali* na watahiniwa 93,089 (6.86%) waliochagua kipotoshi C,


*Wasomaji wa vitabu vingi* nao hawakuwa sahihi kwa sababu kuwa na vipaji vya kucheza michezo mingi na uwezo wa kusoma vitabu vingi ni muhimu kuambatane na kuwa na nidhamu na kujitambua ili kuwafanya wanafunzi kufikia malengo yao. Kwa maana hiyo, nidhamu ndiyo hufanya kipaji cha mwanafunzi kifanikiwe, huku akiendelea kuzingatia masomo na taaluma kwa ujumla.

Mwisho, watahiniwa 99,845 (7.36%) waliochagua kipotoshi E, *Wenye kujiamini wakati wote* hawakuwa sahihi kwasababu kujiamini huwafanya wanafunzi kujikubali, na huwajengea uwezo wa kutawala mwenendo wa maisha yao na kudhibiti mitazamo hasi. Kujiamini bila nidhamu humsababishia mwanafunzi kuwa na kiburi. Kwa hiyo, nidhamu ndio msingi wa kila mafanikio, huleta unyofu, umakini na matumaini katika maendeleo mazuri ya kitaaluma.

**Swali la 28**: Ng'ombe wa Bwana Nguvumali walikufa kutokana na ukame. Bwana Nguvumali aliamua kuiba ng'ombe wa Bwana Kazimoto. Ni tabia ipi Bwana Nguvumali alishindwa kuionesha?

A Uwajibikaji na uvumilivu
B Uvumilivu na wizi
C Uvumilivu na uadilifu
D Uadilifu na ustahimilivu
E Uvumilivu na ukarimu

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mstahimilivu*, na liliwataka watahiniwa kubainisha ulazima wa kuwa na tabia ya uadilifu na ustahimilivu katika jamii. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 188,100 (13.87%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,168,206 (86.13%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Uadilifu na ustahimilivu* walielewa maana ya uadilifu kuwa ni hali ya kuwa mwaminifu na kuwa na kanuni thabiti za maadili. inahusisha kuendelea kufanya yaliyo mema na kudumisha viwango vya maadili vya mtu, hata anapokabiliwa na changamoto au vishawishi. Mtu mwadilifu ana uaminifu, uthabiti, ujasiri wa maadili na mnyofu. Kadhalika, walikuwa wakifahamu kwamba ustahimilivu ni uwezo wa kujikwamua au kukabiliana na dhiki, vikwazo au changamoto. Unahusisha kukabiliana na hali ngumu na kudumisha mtazamo chanya licha ya changamoto zilizopo. Kwa hivyo, mtu mvumilivu ana sifa za kubadilika kulingana na mazingira, matumaini na udhibiti wa mihemko. Chati Na 28 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 28.




**Chati Na 28**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 28*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 332,037 (24.48%) waliochagua kipotoshi A, *Uwajibikaji na uvumilivu* na watahiniwa 406,083 (29.94%) waliochagua kipotoshi C, *Uvumilivu na uadilifu* hawakuelewa kuwa uwajibikaji huashiria wajibu au nia ya kukubali kuwajibika kwa matendo ya mtu. Unahusisha kuwajibika kwa matokeo ya maamuzi na matendo ya mtu. Baadhi ya sifa za uwajibikaji ni uwazi na uaminifu. Vivyo hivyo, uvumilivu ni uwezo wa kukubali au kustahimili maoni, imani au tabia za wengine ambazo ni tofauti na za mtu mwenyewe. Unahusisha kuonesha heshima na uelewa kwa wengine hata kama mtu hakubaliani nao. Sifa za uvumilivu ni pamoja na kuwa na mawazo wazi, subira, huruma na heshima.


Halikadhalika, watahiniwa 185,345 (13.67%) waliochagua kipotoshi B, *Uvumilivu na wizi* walipotoka kwakuwa wizi ni kitendo cha kuchukua mali ya mtu mwingine bila idhini yake, kwa nia ya kuchukua kabisa; jambo ambalo ni kosa la jinai na ni kinyume cha maadili. Sifa za wizi ni pamoja na kukosa uaminifu, uadilifu na huruma. Mwisho, watahiniwa 231,822 (17.09%) waliochagua kipotoshi E, *Uvumilivu na ukarimu* hawakujua kuwa ukarimu unarejelea mapokezi ya urafiki na kuwaburudisha wageni. Hujumuisha kuunda mazingira ya kukaribisha na yenye kufariji kwa wengine. Pia,sifa zake ni pamoja na usikivu na  kuonesha huruma.

**Swali la 29**: Kila mtu ana majukumu ya kutekeleza katika jamii. Jukumu gani kuu wanafunzi wanatakiwa kulitekeleza shuleni?

A Kusoma masomo yote kwa bidii
B Kushiriki katika michezo shuleni
C Kukimbia mchakamchaka
D Kumwagilia bustani ya shule
E Kusafisha eneo la shule

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na liliwataka watahiniwa kubaini majukumu ambayo wanafunzi wanatakiwa kuyafanya wakiwa shuleni. Swali hili lilifanywa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 1,035,388 (76.34%) walijibu kwa usahihi ukilinganisha na watahiniwa 320,918 (23.66%) walioshindwa kujibu kwa usahihi. Jibu sahihi lilikuwa A, *Kusoma masomo yote kwa bidii,* na watahiniwa waliolichagua walielewa dhana ya uwajibikaji kuwa ni wajibu au takwa la kufanya jambo pasipo hiari. Wajibu unahusisha kuchukua umiliki wa matendo ya mtu na kufanya uamuzi. Walijua baadhi ya majukumu ya wanafunzi kama vile kuhudhuria shule mara kwa mara na kwa wakati, kujiandaa kwa ajili ya masomo, kushiriki darasani, kukamilisha kazi za shuleni, kufuata sheria na kanuni za shule, kuonesha heshima kwa wengine, kutunza mali za shule, kushiriki katika shughuli za ziada na kujenga mazoea mazuri ya kujifunza.

Zaidi ya hayo, walielewa umuhimu wa majukumu katika mafanikio ya kitaaluma kuwa ni pamoja na uwajibikaji, maendeleo ya kijamii na maadili ya kujenga uaminifu, ukuaji wa kibinafsi na ujenzi wa jamii. Chati Na 29 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 29.




**Chati Na. 29**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 29*


Kwa upande mwingine, watahiniwa waliochagua kipotoshi B, *Kushiriki katika michezo shuleni* 48,458 (3.57%), C, *Kukimbia mchakamchaka* 50,705 (3.74%), D, *Kumwagilia bustani ya shule 38,752* (2.86%) na E, *Kusafisha eneo la shule 173,142* (12.77%), hawakuelewa kwamba vipotoshi vyote B, C, D na E ni shughuli za mtaala wa ziada. Kiuhalisia, wanafunzi wanawajibika kushiriki katika shughuli mbalimbali za kimichezo kama vile mashindano ya madarasa katika mchezo wa mpira wa miguu, kukimbia mchakamchaka asubuhi ili kuimarisha afya zao, kumwagilia bustani za shule pamoja na kusafisha mazingira ya shule ili yawe mazuri kwa ujifunzaji na ufundishaji. Watahiniwa walitakiwa kuelewa kuwa shughuli zote hizo wanafunzi hupangiwa kama majukumu ya ziada kwa lengo la kuwaandaa kuwa wawajibikaji wanaokubalika katika jamii. Hivyo, vipotoshi vyote havikustahili kuwa majukumu makuu ya mwanafunzi shuleni.

**Swali la 30**: Ni muhimu sana kwa wanafunzi kutekeleza majukumu ya nyumbani. Ni kwa namna gani wanafunzi wanaweza kuongeza ufanisi katika utendaji wa shughuli za nyumbani?

A Kutumia ratiba ya shuleni kufanya shughuli za nyumbani
B Kufanya kazi kwa bidii shuleni tu
C Kutokwenda shule hadi akamilishe shughuli zote za nyumbani
D Kufanya tathmini ya utendaji wa majukumu yote ya nyumbani
E Kufanya majukumu ya nyumbani usiku kucha

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mstahimilivu* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini njia za kuongeza ufanisi kwa mwanafunzi katika utendaji wa shughuli za nyumbani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 853,465 (62.93%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 502,841 (37.07%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi D, *Kufanya tathmini ya utendaji wa majukumu yote ya nyumbani* walielewa kuwa kutathmini kunamaanisha mchakato wa kukusanya, kuchambua, na kutafsiri taarifa ili kufanya uamuzi kuhusu ujifunzaji na utendaji. Madhumuni ya tathmini kwa muktadha huu ni kutoa mrejesho juu ya maendeleo au utendaji wa mwanafunzi. Tathmini ina idadi ya majukumu ya kutekeleza kwa ufaulu wa mwanafunzi kama vile mrejesho kuhusu ujifunzaji au utendaji, motisha, mwongozo wa kuboresha,

kujitambua, uwajibikaji na tathmini ya mapungufu ya ujifunzaji au utendaji. Watahiniwa hao walielewa kuwa ili kuboresha utendaji kazi wa kazi za nyumbani, wanafunzi wanahitaji kuweka malengo wazi, kuweka vipaumbele vya kazi katika hatua ndogo ndogo na kufanya mazoezi ya kujitunza. Tathmini ya majukumu ni muhimu kwa kudumisha na kuboresha utendaji kazi ili kufikia malengo, kufanya maamuzi sahihi, kukuza uwajibikaji na ukuaji katika nyanja mbalimbali za maisha kwa ujumla. Chati Na. 30 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 30.




**Chati Na. 30**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 30*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 286,694 (21.14%) waliochagua kipotoshi A, *Kutumia ratiba ya shuleni kufanya shughuli za nyumbani* na watahiniwa 73,008 (5.38%) waliochagua kipotoshi B, *Kufanya kazi kwa bidii shuleni tu* hawakuelewa kuwa shughuli za nyumbani ni tofauti na shughuli au majukumu ya kila siku shuleni na kwamba ratiba ya shuleni haiwezi kutumika kutekeleza shughuli za nyumbani. Shughuli za nyumbani ni pamoja na kusaidia kuwalea wadogo zake, kuhudumia mifugo, kutunza rasilimali za nyumbani, kupika, kupiga pasi, kuosha vyombo, na kufua nguo; na shughuli za kila siku. Shughuli za shuleni ni pamoja na kuhudhuria vipindi, kusafisha madarasa, kusafisha mazingira ya shule, kuandika nukuu za masomo, na zingine kama hizo. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa baadhi ya shughuli za nyumbani huhitaji


maelekezo maalum na uzoefu, hivyo kufanya kazi kwa bidii shuleni peke yake hakuwezi kuongeza ufanisi wa majukumu ya nyumbani.

Aidha, watahiniwa 86,439 (6.37%) waliochagua kipotoshi C, Kutokwenda *shule hadi akamilishe shughuli zote za nyumbani na* watahiniwa 43,569 (3.21%) waliochagua kipotoshi E, *Kufanya majukumu ya nyumbani usiku kucha* wote hawakuwa sahihi. Mfano wa majukumu ya nyumbani ni kama vile kupika na kuosha vyombo, na hufanyika katika mazingira ya nyumbani. Vilevile, watahiniwa hao walishindwa kutambua kuwa majukumu ya nyumbani hayawezi kumalizika katika usiku mmoja kwa kuwa ni utaratibu wa kawaida wa kazi.

**Swali la 31**: Babulee alikataa kwenda kuwinda ndege na rafiki zake kwa kuwa ulikuwa muda wa kipindi cha Hisabati. Alipoulizwa alijibu kwamba alipima faida na hasara za jambo hilo ndipo alifanya uamuzi. Kitendo hiki kinaitwaje?

A Tathmini ya kina
B Mawazo ya kina
C Uamuzi sahihi
D Mapendekezo sahihi
E Uchambuzi wa kina

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mstahimilivu* na lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya umuhimu wa tathmini katika kufanya maamuzi sahihi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 479,698 (35.37%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 876,608 (64.63%) hawakulijibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Tathmini ya kina*, walikuwa wanafahamu kwamba tathmini ni uchunguzi maalumu wa kitu ili kubaini thamani, ubora au umuhimu wake. Inahusisha kutathmini uwezo na udhaifu wa somo au hali. Inatoa msingi wa kufanya maamuzi sahihi na maboresho. Zaidi ya hayo, inaboresha ufanyaji maamuzi, utatuzi wa matatizo, inapima maendeleo na mwongozo wa hatua. Chati Na 31: inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 31.




**Chati Na 31**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 31*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 177,116 (13.06%) waliochagua kipotoshi B, *Mawazo ya kina* hawakujua kwamba dhana hii inahusu maoni ya mawazo, au mchakato wa kiakili unaotokea ndani ya akili. Ni msingi wa kutatua matatizo na ubunifu. Kukusanya na kupanga mawazo kunaweza kusababisha maamuzi sahihi. Mawazo ya kina yakizingatiwa na kufanywa kwa utaratibu humsaidia mtoa maamuzi kufikia uamuzi wa busara. Hivyo, mawazo ya kina hayawezi kuwa msaada kama hayajapangiliwa kwa utaratibu na kwa lengo lililokusudiwa ili kumfanya mhusika afanye maamuzi.


Vivyo hivyo, watahiniwa 488,455 (36.01%) waliochagua C, *Uamuzi sahihi* hawakujua kuwa dhana hiyo inamaanisha chaguzi/maamuzi yaliyofanywa kati ya mambo zaidi ya moja ikiwa ni njia mbadala au hatua ya kuchukua. Zinajumuisha kuchagua chaguo moja kati ya nyingine ili kufikia lengo maalumu. Hivyo, maamuzi sahihi hayawezi kuwa sawa na tathmini ya kitu au jambo. Pia watahiniwa 121,118 (8.93%) waliochagua kipotoshi E, *Uchambuzi wa kina* hawakuwa sahihi kwa sababu ni mchakato wa kuchunguza data, taarifa au tatizo kwa undani ili kuelewa vipengele vyake, mahusiano na athari zake. Inahusisha kugawanya masuala magumu katika sehemu ndogo zinazoweza kudhibitiwa zaidi. Inasaidia kutambua mifumo, mienendo na ufumbuzi unaowezekana.

Mwisho, watahiniwa 76,044 (5.61%) waliochagua kipotoshi D, *Mapendekezo sahihi,* hawakuwa sahihi kwani mapendekezo yanarejelea ushauri unaotolewa kwa kuzingatia uchanganuzi au utaalamu. Katika muktadha huu, pendekezo linaweza kusababisha chaguzi zenye ufahamu zaidi na bora, hasa katika hali ngumu au isiyojulikana. Mapendekezo sahihi hayawezi kusaidia kufanya maamuzi yenye tija.

**Swali la 32**: Tabia ya unafiki katika jamii ni jambo lisilofaa kutokana na athari zake hasi. Kipi kifanyike ili kuiondoa katika jamii?

A Kushitaki wanafiki mahakamani
B Kuhoji wanafiki mbele ya umma
C Kueleza ukweli kuhusu wanafiki
D Kusuta wanafiki mbele ya umma
E Kuwatenga wanafiki na watu wengine

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwadilifu* na liliwataka watahiniwa kubaini njia za kuondoa unafiki katika jamii. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 850,890 (62.74%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 505,416 (37.26%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi C, *Kueleza ukweli kuhusu wanafiki* walikuwa wanafahamu tabia ya unafiki kama kitendo cha kujifanya kuwa na imani, fadhila au kanuni za maadili ambazo mtu hana au kuishi nazo. Inahusisha kutengana kati ya kile mtu anachokisema na kile anachokifanya, mara nyingi kwa nia ya kuwadanganya wengine au kuepuka kukosolewa. Hutokea pale mtu anapofanya mambo kinyume na anayoyasema (sio mkweli). Pia, walielewa kuwa wanafiki wanafanya undumilakuwili, udanganyifu, kutofautiana, maslahi binafsi na ukosefu wa uwajibikaji. Watahiniwa hao walitambua kuwa tabia ya unafiki haikubaliki kwani ina matokeo mabaya. Matokeo kama haya yanajumuisha mmomonyoko wa uaminifu, kudhoofisha uadilifu, migogoro na chuki, kupungua kwa uaminifu na uadilifu katika jamii. Na inaweza kuwa chanzo cha msongo wa kisaikolojia. Chati Na. 32 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 32.




**Chati Na. 32**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 32*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 125,393 (9.25%) waliochagua kipotoshi A, *Kushitaki wanafiki mahakamani* hawakuwa sahihi kwani ni vigumu kutumia misingi ya kisheria kuwashitaki wanafiki mahakamani. Watahiniwa hao walikosa uelewa kuwa tabia ya mtu ya ndani kama vile hisia, imani na mitazamo haviwezi kuamuliwa kwa muonekano au matendo yanayo jidhihirisha kwa nje. Vilevile, watahiniwa 184,139 (13.58%) waliochagua kipotoshi B, *Kuhoji wanafiki mbele ya umma* na watahiniwa 80,787 (5.96%) waliochagua kipotoshi D, *Kusuta wanafiki mbele ya umma* wote hawakuwa sahihi kwani kuwahoji au kuwasuta wanafiki mbele ya umma ni kitendo cha uzalilishaji ambacho hushusha utu wao au heshima yao katika jamii. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa kuwa tabia ya unafiki ndiyo inayopaswa kukemewa au kupingwa hadharani na sio watu.


Aidha, watahiniwa 101,854 (7.51%) waliochagua kipotoshi E, *Kuwatenga wanafiki na watu wengine* hawakuwa sahihi kwa sababu kitendo cha watu kujumuika katika shughuli za kila siku hakiepukiki na mikusanyiko ya kijamii. Hivyo, kuwatenga wanafiki mbali na wanajamii wengine sio suluhisho la tabia ya unafiki. Wanafiki wanahitaji kuelimishwa juu ya matokeo ya tabia yao kwao wenyewe na jamii kwa ujumla.

**Swali la 33**: Rushwa ni adui wa haki za watu na maendeleo. Madhara ya rushwa katika jamii ni yapi ?

A Kupata wataalamu wasio na sifa
B Kupata wahitimu wengi
C Kushuka kwa bei za bidhaa
D Kushuka kwa idadi ya vifo
E Kukosekana kwa matabaka katika jamii

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwadilifu* na liliwataka watahiniwa kutathmini athari za rushwa katika jamii. Swali hili lilifanywa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 625,276 (46.10%) walitambua jibu sahihi na watahiniwa 731,030 (53.90%) walishindwa. Watahiniwa waliotambua jibu sahihi A, *Kupata wataalam wasio na sifa* lilichaguliwa na watahiniwa ambao walijua maana ya rushwa kuwa ni matumizi mabaya ya mamlaka ya umma au rasilimali kwa manufaa ya binafsi, kuwa mara nyingi kwa njia zisizo za kimaadili au zisizo halali. Rushwa ni kikwazo kikuu cha kupatikana haki na maendeleo ya watu. Hivyo, rushwa inaondoa uaminifu na imani, inadhoofisha maendeleo ya kiuchumi, ukosefu wa usawa na husababisha umaskini, mgawanyo usiofaa wa rasilimali, utawala dhaifu wa sheria, kudhoofisha huduma za umma na kuchochea vitendo vya uhalifu.

Aidha, walijua kwamba rushwa inaweza kukabiliwa kwa kufanya vitendo vya uwazi, uwepo wa sheria za kupambana na rushwa, kuimarisha taasisi, elimu kwa umma, uhamasishaji na uwajibikaji wa shirika au taasisi. Chati Na 33 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 33.




**Chati Na. 33**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 33*

Hata hivyo, chaguo B, *Kupata wahitimu wengi* lilichaguliwa na watahiniwa 87,578 (6.46%) ambao hawakuweza kung'amua kwamba kupata wahitimu wengi ni matokeo ya mambo mtambuka ambayo hayawezi kusababishwa na rushwa tu. Kupata wahitimu wengi kunaweza kuwa ni matokeo ya sababu mbalimbali. Kwa mfano, kupanuka kwa miundombinu ya elimu ambayo imeruhusu kudahili wanafunzi wengi au utoaji wa elimu bila malipo ambao umewezesha watu wengi kupata huduma za elimu, hivyo kuwa na wahitimu wengi.

Vivyo hivyo, watahiniwa, 179,793 (13.26%) waliochagua kipotoshi C, *Kushuka kwa bei za bidhaa*, hawakuzingatia ukweli kwamba kushuka kwa bei za bidhaa ni kiashiria cha kutokuwepo kwa mazingira ya rushwa katika uzalishaji pamoja na uendeshaji wa biashara. Pili, watahiniwa hawakuweza kutambua sababu mbalimbali ambazo husababisha bei za bidhaa kubadilika mara kwa mara kama vile hali ya mahitaji na usambazaji bidhaa, matukio ya kijografia, majanga ya asili, gharama za uzalishaji na matumizi katika biashara, ushindani na sera za serikali. Kwa hiyo, katika muktadha huu vipotoshi B na C havikustahili kuwa majibu sahihi.

Zaidi ya hapo, watahiniwa wengine 76,811 (5.66 %) walichagua kiposhi D, *Kushuka kwa idadi ya vifo*. Hao hawakutambua kwamba rushwa huongeza uwezekano wa kuongeza idadi ya vifo kuliko kuvipunguza. Kwa mfano, katika hali ya kawaida, wafanyakazi katika sekta ya afya wakiwa wala rushwa inategemewa kuwa watu ambao hufa kwa kucheleweshewa au kwa kukosa madawa, au matibabu stahiki huogezeka. Hata hivyo, kupungua kwa idadi ya vifo husababishwa na mambo mbalimbali kama vile uwezo wa kukabiliana na majanga ya asili, kudhibiti magonjwa, ajali, uelewa juu ya masuala ya afya na kudhibiti uchafuzi wa mazingira.


Vilevile, kipotoshi E, *Kukosekana kwa matabaka katika jamii,* lilichaguliwa na watahiniwa 371,479 (27.39%) ambao walipuuzia mchango wa rushwa katika kutengeneza matabaka katika jamii. Hawakutambua kuwa rushwa inaposhamiri katika nchi, kunakuwa na uwezekano wa kutengeneza matabaka hasimu makubwa mawili: tabaka la wanaofaidika na waathirika wa vitendo vya rushwa. Katika hali hii, rushwa huongeza uwezekano mkubwa wa matabaka ya kijamii. Kwa hiyo, kipotoshi hiki hakikustahili kuwa jibu sahihi.

**Swali la 34**: Ukweli na uwazi ni tabia muhimu katika jamii, ingawa baadhi ya wanajamii huzipuuza. Njia zipi zitumike ili kuboresha tabia hizi?

A Kushauri watu kuwa wastahimilivu na wanyenyekevu
B Kuwaelekeza watu kuongea ukweli na kukataa maovu
C Kusisitiza uaminifu kwa viongozi
D Kufuata mawazo ya wazee katika jamii
E Kufuata miongozo ya viongozi waliopo

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mwadilifu*, na lilipima uelewa wa watahiniwa juu ya umuhimu wa tabia ya ukweli na uwazi katika jamii. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 642,201 (47.35%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 714,105 (52.65%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Kuwaelekeza watu kuongea ukweli na kukataa maovu* walielewa kwamba ukweli ni hali au ubora wa kuwa na uhakika wa jambo. Unahusisha uaminifuna usahihi katika mawasiliano na matendo.

Zaidi ya hayo, uwazi unarejelea desturi ya kufanya taarifa, taratibu na maamuzi kupatikana na kueleweka kwa urahisi na umma. Unahusisha uwazi uwajibikaji, na mawasiliano ya wazi. Kando na hayo, watahiniwa walifahamu faida zinazotokana na uwazi na ukweli kwa jamii yenye afya na utendaji kazi. Faida katika jamii ni pamoja na kuongezeka kwa uaminifu, kupungua kwa migogoro, kufanya maamuzi bora na hali ya usawa. Tabia hizi husaidia kudumisha utulivu wa kijamii, kukuza haki, na kuhakikisha kwamba haki na mahitaji ya watu binafsi yametimizwa. Chati Na. 34: inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 34.




**Chati Na. 34**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 34*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 401,000 (29.57%) waliochagua kipotoshi A, *Kushauri watu kuwa wastahimilivu na wanyenyekevu* hawakujua kwamba kuwa na ustahimilivu na unyenyekevu sio njia za kukuza ukweli na uwazi; kwa sababu ustahimilivu ni uwezo wa mtu binafsi kustahimili changamoto anazopitia na kuwa mnyenyekevu ni hali ya kuwa na heshima na utulivu fulani au tabia iliyojengeka. Hivyo, unyenyekevu ni sifa ya kuwa mwenye kiasi au asiye na makuu.

Aidha, watahiniwa 126,154 (9.30%) waliochagua kipotoshi C, *Kusisitiza uaminifu kwa viongozi* hawakuwa sahihi kwani kuwa mkweli kunamaanisha kuweza kuaminiwa pasi uwezekano wa kuiba, kudanganya au kusema uongo. Msisitizo ni wajibu wa kudumisha maadili kwa watu wote, ikiwa ni pamoja na viongozi wa juu wa serikali na kwa jamii nzima.

Vilevile, watahiniwa 88,506 (6.53%) waliochagua kipotoshi D, *Kufuata mawazo ya wazee katika jamii* na watahiniwa 83,370 (6.15%) waliochagua E, *Kufuata miongozo ya viongozi waliopo* nao hawakuwa sahihi. Watahiniwa hawa hawakujua kwamba, pamoja na ukweli kuwa wazee wana uzoefu wa maisha na viongozi wana mamlaka juu ya mambo kadhaa katika jamii; baadhi wana changamoto ya kutozingatia maadili. Mathalani,


baadhi ya wazee ni walevi, matapeli na baadhi ya viongozi ni wala rushwa. Kwa hiyo, jamii haiwezi kuegemea maoni na maelekezo ya haya makundi moja kwa moja ili kukuza tabia njema katika jamii.

**Swali la 35**: Tanzania inasifika kwa kuwa na uhusiano mzuri na mataifa mengine. Ipi ni misingi ya Tanzania kuhusu sera ya mambo ya nje ?

A Usawa na utu
B Uhuru na ujamaa
C Uwazi na ukweli
D Mshikamano na uvumilivu
E Uhuru na kujitegemea

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha amani*, na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu misingi ya sera ya mambo ya nje ya Tanzania. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 203,297 (14.99%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 1,153,009 (85.01%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Usawa na utu* walijua kuwa Tanzania inatambua misingi yake ya sera ya mambo ya nje. Walijua kuwa usawa unamaanisha kwamba watu wote wanapaswa kutendewa sawa, kupewa fursa na heshima bila kujali sifa zao kama vile rangi, jinsia, dini, hali ya kijamii na kiuchumi, ulemavu, au matabaka yao. Ina maana kwamba kila mtu anapaswa kuwa na nafasi sawa ya kufanikiwa na kuwa huru kutoka kwenye ubaguzi na chuki.

Zaidi ya hayo, utu wa binadamu unajumuisha thamani ya ndani ambayo kila mtu anayo kwa sababu tu ya kuwa binadamu. Ni kwamba kila mtu ana haki ya kuheshimiwa na kulindwa, kupewa mahitaji na haki zake za kimsingi. Masuala mengine yanayohusiana na sera ya mambo ya nje ya Tanzania ni pamoja na kutofungamana na upande wowote, kuwa huru, amani, usalama, na diplomasia ya uchumi. Chati Na 35 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali hili.




**Chati Na. 35**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 35*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 298,863 (22.04%) waliochagua kipotoshi B, *Uhuru na ujamaa*, watahiniwa 139,391 (10.28%)waliochagua kipotoshi E, *Uhuru na kujitegemea*, na watahiniwa 288,680 (21.28%) waliochagua kipotoshi D, *Mshikamano na uvumilivu* hawakuwa sahihi kwa kwa sababu uhuru ni hali ya kuwa na uwezo wa kutenda na kufanya mambo bila vikwazo vya nje, shuruti, au kuingiliwa. Ni tunu ya msingi ya binadamu inayohusishwa na kanuni za demokrasia na haki za binadamu.


Aidha, ujamaa ni itikadi ya kiuchumi na kisiasa inayotetea umiliki wa pamoja au wa serikali na udhibiti wa njia za uzalishaji mali. Kujitegemea ni uwezo na utayari wa mtu binafsi, jumuiya, au taifa kukidhi mahitaji yao ya msingi, kufanya maamuzi na kutatua matatizo bila kutegemea msaada au rasilimali kutoka nje. Kwa wale waliochagua mshikamano hawakujua kwamba mshikamano unaashiria hali ya umoja, ushirikiano, na kusaidiana kati ya watu binafsi au vikundi, hasa wakati wa shida au changamoto. Unahasisha watu kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya wahitaji. Uvumilivu unahusisha kuonesha heshima na uelewa kwa wengine hata kama mtu hakubaliani nao. Mwisho, watahiniwa 409,915 (30.22%) waliochagua kipotoshi C, *Uwazi na ukweli* hawakujua kuwa uwazi na ukweli ni nguzo za utawala bora ambazo nchi inazizingatia ili kuleta uwajibikaji katika utendaji

wa serikali kwa madhumuni ya kukuza demokrasia na utengamano katika taifa. Umuhimu wake umetokana na imani, uwajibikaji na usawa.

**Swali la 36**: Umoja wa Mataifa ni chombo kinachojumuisha mataifa huru duniani. Jambo gani lilichangia kuanzishwa kwake?

A Kuzuia Marekani isitawale dunia
B Kuepusha vita nyingine ya dunia isitokee
C Kuandaa mataifa ya Afrika kupata uhuru wao
D Kulinda maslahi ya nchi tajiri duniani
E Kuizuia Uingereza isitawale mataifa ya kiafrika

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na liliwataka watahiniwa kubaini kiini cha kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 630,619 (46.50%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 725,687 (53.50%) hawakujibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Kuepusha vita nyingine ya dunia isitokee* walikuwa wanafahamu malengo na misingi ya Umoja wa Mataifa kuwa ni kuzuia vita vingine vya dunia, kuendeleza amani na usalama wa kimataifa, kukuza haki za binadamu, kuhimiza maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kuratibu ushirikiano wa kimataifa na kuanzisha sheria za kimataifa. Kwa ujumla, Umoja wa Mataifa ulianzishwa ili kutoa majibu ya pamoja kwa changamoto zinazoikabili dunia na kukuza amani, usalama na ustawi kwa watu wote. Chati Na. 36 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 36.




**Chati Na. 36**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 36*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 100,267 (7.39%) waliochagua kipotoshi A, *Kuzuia Marekani isitawale dunia* hawakuelewa kuwa Marekani ilikuwa na nguvu kubwa sana kijeshi na kiuchumi pamoja na ushawishi wa jumla. Watahiniwa hao walishindwa kutambua kwamba Marekani isingeweza kutawala dunia kwa sababu kulikuwa na mataifa mengine yenye nguvu sawa ya kiuchumi. Pia, malengo ya ulimwengu yamebadilika sana kwa kiwango ambacho Marakeni haiwezi kutawala ulimwengu kwa njia za kizamani.

Aidha, watahiniwa 337,223 (24.86%) waliochagua kipotoshi C, *Kuandaa mataifa ya Afrika kupata uhuru wao* hawakuwa sahihi kwa sababu nchi za Kiafrika zote ziko huru kutoka kwenye utawala wa kikoloni na jumuiya ya Umoja wa Mataifa halijatimiza malengo yake ya awali. Watahiniwa hao hawakufahamu kuwa, mbali na kuhimiza amani na usalama duniani, Umoja wa Mataifa kupitia mashirika yake mbalimbali umejizatiti katika kuendeleza misaada ya kibinadamu na kiuchumi duniani. Hii inatekelezwa kupitia mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa kama vile *UNICEF, WHO, UNHCR* na *UNDP.*

Vilevile, watahiniwa 93,411 (6.89%) waliochagua kipotoshi D, *Kulinda maslahi ya nchi tajiri duniani* hawakuwa sahihi kwa sababu Umoja wa Mataifa unaundwa na nchi tajiri na maskini zenye maslahi na matamanio mbalimbali. Umoja wa Mataifa unaongozwa na kanuni kadhaa kama vile wanachama wote kutimiza kwa nia njema majukumu wanayochukua kwa mujibu wa katiba, kutatua migogoro yao ya kimataifa kwa njia ya amani kwa namna ambayo amani na usalama wa kimataifa na haki hazihatarishwi.


Pia, watahiniwa 177,621 (13.10%) waliochagua kipotoshi E, *Kuizuia Uingereza isitawale mataifa ya kiafrika*, hawakuwa sahihi kwani nchi za kiafrika zilitawaliwa na mataifa kadhaa ya Ulaya ikiwemo Uingereza. Hivyo haikuwa sababu ya kuanzishwa kwa Umoja wa mataifa. Hivyo, ni kweli kwamba hali ya sasa hairuhusu kuwepo kwa aina ya ukoloni wa kizamani.

**Swali la 37**: Ni mila ipi potofu humsababishia mama mjamzito kutokwa damu nyingi au kupoteza maisha wakati wa kujifungua?

A Kuzuia wanawake kula baadhi ya vyakula
B Ukeketaji kwa wanawake
C Mwanamke kufanya kazi nyingi
D Kuwa na jukumu la kuhudumia familia
E Kurithi wajane

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na liliwataka watahiniwa kutambua mila potofu ambayo humsababishia mama mjamzito kutokwa damu nyingi au kupoteza maisha wakati wa kujifungua. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 105, 5461 (77.82%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 300,845 (22.18%) walijibu isivyo sahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Ukeketaji kwa wanawake*, walikuwa wakizifahamu mila za kitamaduni zilizopitwa na wakati kwa wanawake kama vile mila ambazo zimekuwa zikifanywa kutoka vizazi hadi vizazi katika jamii, lakini zinaenda kinyume na haki za binadamu, usawa wa kijinsia, au uwezeshaji wa wanawake. Watahiniwa walijua kuwa ukeketaji unarejelea kuondolewa kwa sehemu au jumla ya viungo vya nje vya mwanamke kwa sababu zisizo za kimatibabu. Baadhi ya madhara ni pamoja na kutokwa na damu nyingi, maumivu na mshtuko wakati wa kufanyiwa upasuaji, matatizo wakati wa kujifungua, kushindwa kufanya ngono na kupungua kwa hamu ya kujamiana, na hata kunyanyapaliwa na kutengwa kwa wanawake ambao hawajakeketwa. Aina nyingine za tamaduni zilizopitwa na wakati nchini Tanzania ni pamoja na ndoa za utotoni, urithi wa wajane, ukatili wa kijinsia, ulipaji wa mahari, na tuhuma za uchawi. Juhudi za kutokomeza ukeketaji zinahusisha mchanganyiko wa sheria, elimu, ushirikishwaji wa jamii, na usaidizi wa desturi mbadala za kitamaduni.

Kwa ujumla, mila na desturi zilizopitwa na wakati kwa wanawake zinaweza kudhibitiwa kupitia sheria, ufahamu na elimu, uwezeshaji na fursa za kiuchumi, ushirikishwaji wa jamii, usaidizi wa kisheria na utetezi. Chati Na 37 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 37.




**Chati Na. 37**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 37*

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa 81,319 (6.00%) walichagua kipotoshi A, *Kuzuia wanawake kula baadhi ya vyakula*. Watahiniwa hawa hawakuelewa kuwa hicho ni kitendo cha kuwanyima wanawake haki ya kula vyakula vyenye virutubisho muhimu kama vile mayai na maini. Mila hii husababisha ukosefu wa lishe muhimu mwilini au utapiamlo kwa mama na mtoto anayetarajiwa kuzaliwa. Licha ya hivyo, hali hii haiwezi kumsababishia mama mjamzito kupoteza damu nyingi au kupoteza maisha wakati wa kujifungua. Vivyo hivyo, watahiniwa 97,885 (7.22%) waliochagua kipotoshi C, *Mwanamke kufanya kazi nyingi* na kipotoshi D, *Kuwa na jukumu la kuhudumia familia 47,819* (3.53%), hawakutambua kuwa vitendo vyote hivyo havikuwa mila potofu. Pia, watahiniwa hawakujua ukweli kuwa vipotoshi vyote viwili vinamaanisha majukumu yanayoweza kufanywa na wanawake wengi katika familia zao. Majukumu haya yanaweza kuhatarisha maisha ya mama mjamzito. Hivyo, ni dhahiri kuwa hayo hayawezi kuwa majibu sahihi.

Mwisho, watahiniwa 62,364 (4.60%) waliochagua kipotoshi E, *Kurithi wajane*, hawakuelewa kwamba ni mila potofu inayomtaka mwanamke aliyefiwa na mume wake kuolewa na ndugu wa karibu wa aliyekuwa mume wake. Kurithi wajane kuna madhara mbalimbali yakiwa ni pamoja na kuongezeka na kuenea kwa maambukizi ya magonjwa kwa njia ya zinaa na UKIMWI. Kwa hiyo, watahiniwa walishindwa kutofautisha madhara ya ukeketaji kwa wanawake na athari za kurithi wajane. Kitendo cha kurithi


wajane hakisababishi mwanamke kutokwa damu anapojifungua ijapokuwa ni mila potofu.

**Swali la 38**: Tanzania ni mwanachama wa jumuiya ya madola. Jumuiya hiyo inaundwa na wanachama waliowahi kutawaliwa na nchi gani ?

A Ufaransa
B Uingereza
C Ureno
D Ubelgiji
E Ujerumani

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na liliwataka watahiniwa kutambua nchi ambayo iliwahi kuzitawala nchi zinazounda Jumuiya ya Madola. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 kati ya hao, watahiniwa765, 606 (56.45%) walijibu kwa usahihi na watahiniwa 590,700 (43.55%) walilijibu visivyo sahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi B, *Uingereza,* walikuwa wanafahamu usuli wa kihistoria wa Jumuiya ya Madola kama muungano wa hiari wa mataifa huru yenye mamlaka kamili. Uhusiano wa kihistoria, maadili ya pamoja, na kuzingatia kanuni na malengo ya kawaida huunganisha nchi hizi wanachama.

Idadi kubwa ya nchi wanachama zilitawaliwa na Uingereza ingawa nchi nyingine zilijiunga na jumuiya hiyo bila kuwa na historia na Uingereza. Madhumuni ya msingi ya kuanzishwa kwake ni kama vile kudumisha amani na usalama, kukuza demokrasia, kulinda haki za binadamu, maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi, kubadilishana utamaduni na elimu, na maendeleo endelevu. Kwa hali hiyo, jumuiya ya madola ina jukumu muhimu katika kukuza ushirikiano, amani, maendeleo, na maadili ya pamoja kati ya nchi wanachama. Inatoa jukwaa kwa nchi kushirikiana katika masuala mbalimbali ya kimataifa na kuyafanyia kazi kwa mustakabali ulio sawa na endelevu. Chati Na 38 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 38.




**Chati Na. 38**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 38*

Hata hivyo, Vipotoshi A, *Ufaransa* 83,309 (6.14%), C, *Ureno* 119,996 (8.85%), D, *Ubelgiji* 88,830 (6.55%) na E, *Ujerumani* 281,367 (20.75%) vilichaguliwa na watahiniwa ambao hawakuwa na uelewa juu ya masuala ya Jumuiya za Kimataifa, hasa historia inayohusu chimbuko la Jumuiya ya Madola. Watahiniwa hawa hawakutambua kwamba nchi zilizotajwa siyo sehemu ya nchi ya Uingereza ingawa zimewahi kutawala baadhi ya nchi katika sehemu mbalimbali duniani. Kwa muktadha huo, vipotoshi vyote A, C, D na E havikuakisi ukweli wa historia ya Jumuiya ya Madola.


**Swali la 39**: Kuchangamana na watu wenye tamaduni na asili tofauti ni jambo la msingi kwa nchi yoyote. Kuna umuhimu gani wa kuishi na watu wenye asili tofauti?

A Wanatuwezesha kubadilishana ujuzi
B Wanatusaidia kupuuza tamaduni za kigeni
C Wanatusaidia kulinda uzalendo wetu
D Wanatuwezesha kusahau historia za kigeni
E Wanatuhamasisha kulinda tamaduni za asili

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani*, na liliwataka watahiniwa kubainisha umuhimu wa nchi kuchangamana na watu wenye tamaduni na asili tofauti. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 727,192 (53.62%) walijibu swali hili kwa usahihi na

watahiniwa 629,114 (46.38%) hawakulijibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi, A, *Wanatuwezesha kubadilishana ujuzi* walikuwa sahihi kwa vile walielewa kuwa kuishi na watu kutoka tamaduni na malezi tofauti kunahusisha kutangamana na watu ambao wana maadili, mila, lugha na mitazamo mbalimbali ya ulimwengu. Baadhi ya vipengele muhimu na manufaa ya kuishi na watu kutoka tamaduni na asili tofauti ni pamoja na kubadilishana tamaduni, mitazamo iliyopanuka, kujifunza lugha, ujuzi ulioimarishwa wa kutatua matatizo, kuimarisha utamaduni, kujenga mtandao wa kimataifa, ujuzi wa mawasiliano kati ya tamaduni, mchango wa kiuchumi, ushirikiano wa kijamii, uvumbuzi, ubunifu na ukuaji wa binafsi.

Hata hivyo, watu wenye tamaduni na asili tofauti huleta changamoto zinazohusiana na ushirikiano kama vile migongano ya kitamaduni, na uwezekano wa ubaguzi. Watu wa tamaduni na asili tofauti ni muhimu katika nchi kwa mchango wao katika utofauti, utamaduni, uchumi, mshikamano wa kijamii na mitazamo ya kimataifa. Chati Na 39 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 39.




**Chati Na. 39**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 39*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 115,510 (8.52%) waliochagua kipotoshi B, *Wanatusaidia kupuuza tamaduni za kigeni* na watahiniwa 69,412 (5.12%) waliochagua kipotoshi D, *Wanatuwezesha kusahau historia za*

*kigeni* hawakuwa sahihi. Kuchangamana na watu wenye asili tofauti hakuna dhamira ya kudunisha tamaduni zao kwani kuna tamaduni zinazofaa kuigwa. Aidha, hakulengi kuathiri maarifa ya mtu aliyonayo juu ya historia ya kigeni. Kiuhalisia, watu wanachangamana na mataifa mengine huku wakiwa wakiendeleza tamaduni na asili zao huku wakiheshimu haiba na asili zao.


Vilevile, watahiniwa 179,793 (13.26%) waliochagua kipotoshi C, *Wanatusaidia kulinda uzalendo wetu* na watahiniwa 249,195 (18.37%) waliochagua kipotoshi E, *Wanatuhamasisha kulinda tamaduni za asili* nao hawakuwa sahihi kwa sababu uzalendo unajengwa kwa kutunza na kulinda historia ya nchi. Pia, huhusisha kusherehekea sikukuu zetu za kitaifa, kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo, kutetea mamlaka yake na kudumisha hisia zetu za upendo, kujitolea, na hali ya kushikamana na nchi yetu.

**Swali la 40**: Njia ipi inaweza kutumika katika kukabiliana na madhara hasi ya utandawazi nchini Tanzania?

A Kuwasikiliza wazazi na kulinda utamaduni wetu
B Kuzikubali tamaduni zingine na kulinda uzalendo wetu
C Kutumia mitandao ya kijamii bila usimamizi
D Kukuza teknolojia ya mawasiliano kutoka nchi zilizoendelea
E Kuhamasisha vijana kuacha kutumia mitandao ya kijamii

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini njia zinazoweza kutumika katika kukabiliana na madhara hasi ya utandawazi nchini Tanzania. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 553,722 (40.83%) walijibu swali hili kwa usahihi na watahiniwa 802,584 (59.17%) hawakulijibu kwa usahihi. Watahiniwa waliochagua jibu sahihi A, *Kuwasikiliza wazazi na kulinda utamaduni wetu* walilielewa vipengele vya utandawazi vinavyohusisha utangamano, muunganiko, teknolojia, ushirika wa mashirika ya kimataifa na kubadilishana utamaduni. Watahiniwa hao walijua kwamba utandawazi unaweza kudhibitiwa kupitia kukuza, kuhifadhi utamaduni, kukuza viwanda vya ndani, kuwekeza katika elimu, na uhamasishaji na ushirikishaji wa umma. Kwa kutekeleza hatua hizi, Tanzania inaweza kufanya kazi ya kupunguza athari mbaya za utandawazi huku ikitumia fursa zinazotolewa kwa ukuaji wa uchumi na maendeleo. Ni muhimu kuweka uwiano unaoruhusu nchi kufaidika na utandawazi huku tukilinda maslahi ya watu

wetu na mazingira . Chati Na. 40 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 40.




**Chati Na. 40** : *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 40*

Kwa upande mwingine, watahiniwa 253,353 (18.68%) waliochagua kipotoshi B, *Kuzikubali tamaduni zingine na kulinda uzalendo wetu* walielewa kuwa ni jambo jema kuipenda na kuwa tayari kuifia nchi yetu. Maelezo hayo yanakuza hisia ya uwajibikaji wa pamoja kwa ustawi wa nchi, na vilevile kusitawisha hisia ya ufahari na heshima kwa maadili ya taifa letu. Hata hivyo, watahiniwa katika kundi hili hawakujua kwamba kukubali aina ya mitindo ya maisha ya wengine kunamaanisha kudhoofisha utamaduni wetu wenyewe, kwa kuwa baadhi ya mazoea, imani na maadili ya watu wengine hayaendani na yetu. Pia, watahiniwa 157,159 (11.59%) waliochagua kipotoshi C, *Kutumia mitandao ya kijamii bila usimamizi* hawakuwa sahihi kwa sababu kutumia mitandao ya kijamii bila udhibiti inaweza kusababisha tabia zisizokubalika miongoni mwa vijana kama vile uvaaji usiokubalika, matumizi ya madawa ya kulevya, kujihusisha na picha za ngono, na matendo mengine ambayo hayaendani na utamaduni wa kitanzania.

Vilevile, watahiniwa 223,855 (16.50%) waliochagua kipotoshi D, *Kukuza teknolojia ya mawasiliano kutoka nchi zilizoendelea* hawakuelewa kuwa Tanzania, kama mojawapo ya nchi zinazoendelea haiwezi kuepuka


kupokea teknolojia ikiwa ni pamoja na teknolojia ya mawasiliano kutoka nchi zilizoendelea. Changamoto ni kwamba, ni kwa kiwango gani teknolojia inayopokelewa ni sahihi kwa mazingira ya kitanzania. Kipotoshi hiki hakikufaa kuwa chaguo sahihi kwa kuwa ugunduzi wa teknolojia umetawaliwa na nchi zilioendelea kiviwanda na kiteknolojia, na huambatana na masharti magumu ya kisiasa na kiuchumi.

Aidha, watahiniwa 151,513 (11.16%) waliochagua kipotoshi E, *Kuhamasisha vijana kuacha kutumia mitandao ya kijamii* walikosa uelewa wa mchango chanya wa mitandao ya kijamii kwa vijana katika kufanya biashara, kujisomea na kufanya mawasiliano kwa ajili ya kujiendeleza, kiuchumi na kijamii. Vijana wanahitaji kujifunza juu ya matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii badala ya kuwazuia kutumia mitandao hiyo. Vijana wanatakiwa kutumia mitandao ya mawasiliano kwa kutunza siri, kuhakiki usahihi wa taarifa, kuheshimu usawa wa binadamu na kusambaza takwimu sahihi.

## 2.2 Sehemu B: Maswali ya Majibu Mafupi


**Swali la 41**: Uhusano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine hutoa fursa mbalimbali. Fursa zipi mbili zinapatikana kutokana na uhusiano huo?

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na lilipima uelewa wa watahiniwa kuhusu fursa ambazo Tanzania inazipata kutokana na uhusiano wa kidiplomasia. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 na uchambuzi ulionesha kuwa watahiniwa 754,692 (55.64%) walipata alama kuanzia 1 hadi 2 na watahiniwa 601,614 (44.36%) hawakujibu kwa usahihi kwa kuwa walipata alama 0. Chati Na.41 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 41.




**Chati Na. 41**: Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 41

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa, watahiniwa 374,225 (27.59%) walipata alama zote. Watahiniwa katika kundi hili walielewa kuwa uhusiano wa kidiplomasia unarejelea mwingiliano rasmi na wa kiofisi kati ya nchi huru mbili au zaidi, mara nyingi huwezeshwa kupitia misheni zao za kidiplomasia au balozi zilizo katika nchi ya kila mmoja. Uhusiano wa kidiplomasia unadumishwa kupitia balozi na wawakilishi wa nchi katika nchi mwenyeji, mabalozi na wafanyakazi wa kidiplomasia, mikataba na makubaliano, mawasiliano ya kidiplomasia na kinga ya kidiplomasia. Taarifa kuhusu fursa kupitia ubalozi zinapatikana kupitia tovuti, televisheni, redio, mitandao ya kijamii, magazeti, majarida na vipeperushi. Watahiniwa hao waliweza kuchambua fursa inazozipata Tanzania kutokana na mahusiano yake ya kidiplomasia kama vile fursa za kibiashara na kiuchumi, usalama na utulivu, mabadilishano ya kitamaduni, ushirikiano wa kisayansi na kiteknolojia, misaada ya kibinadamu na ushawishi wa utetezi, fursa za masomo, misaada ya kifedha. Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini matakwa ya swali la 41.


SWALI LA 41

i) Kusaidia kubadilishana ujuzi

ii) Kupata fursa za kimasomo na kimichezo

**Kielelezo Na. 1.1**: Sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 41


Katika Kielelezo Na.1.1 watahiniwa waliweza kueleza fursa mbili zinazopatikana kutokana na uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine.

Vilevile, watahiniwa 380,467 (28.05%) waliopata alama 1 walidhihirisha mapungufu kama vile kueleza fursa moja tu ambayo Tanzania inaweza kunufaika nayo kutokana na uhusiano wa kidiplomasia na nchi nyingine. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja moja kati ya mbili ambayo ni *kusafirisha bidhaa kutoka Tanzania kwenda nchi zingine*. Vivyo hivyo, watahiniwa wengine walipata alama 1 kwa sababu ya kurudia hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kupata fursa za kibiashara* na *kupata fursa za mauzo* kama hoja mbili tofauti. Mwingine aliandika, *kupata fursa za masomo* na kupata *fursa za huduma za kijamii kama hoja mbili tofauti*. Baadhi ya watahiniwa walichanganya hoja sahihi na hoja zisizo sahihi, hivyo kupata alama 1. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *fursa za uwekezaji* na *fursa za uongozi* na mwingine aliandika *fursa za kielimu na fursa za uongozi.*


Kwa upande mwingine, watahiniwa 601,614 (44.36%) waliopata alama 0 walikosa maarifa juu ya uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine. Watahiniwa hao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na hivyo kueleza mambo tofauti ambayo hayakuwa sehemu ya majibu sahihi. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa walitaja tunu za taifa kama vile *amani, upendo, umoja, utu na uzalendo* wakimaanisha fursa ambazo Tanzania inaweza kuzipata kupitia uhusiano wa kidiplomasia na nchi nyingine. Watahiniwa wengine walitaja tabia zisizokubalika katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *uwepo wa ukatili, uwepo wa rushwa*.

Changamoto nyingine iliyojitokeza ni ukosefu wa maarifa juu ya umahiri uliopimwa katika swali hili, na hivyo baadhi ya watahiniwa walinakili baadhi

ya maneno na sentensi kutoka katika karatasi ya maswali na kuyafanya majibu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alinakili *kuwa mstahimilivu na mwadilifu* ambalo lilikuwa chaguo E katika swali la 11. Sambamba na huyo, mtahiniwa mwingine alinakili *malengo,* hili lilikuwa chaguo D katika swali la 3. Cha kushangaza zaidi, mtahiniwa mmoja alinakili swali la 41 *Uhusiano wa kidiplomasia kati ya Tanzania na nchi nyingine hutoa fursa mbalimbali. Fursa zipi mbili zinapatikana kutokana na uhusiano huo?* Aidha, watahiniwa wengine walitaja maliasili tulizojaliwa ndani ya nchi kwa asili. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *Wanyama Pori*, *madini*. Vilevile, mtahiniwa mmoja alitaja *Tanganyika* na *Zanzibar* nchi mbili zilizoungana kuunda nchi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.* Mwingine alitaja nchi mbili jirani; yaani Tanzania na Kenya. Vielelezo Na. 1.2: (a) na (b) vinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi katika swali la 41.


SWALI LA 41 (1) Kuna fursa ya kumuomba mungu kufaulu na ukapata
(1) Fursa ya kumuomba mungu kupata kibarua


**Kielelezo Na. 1.2 (a)**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyeshindwa Kujibu Swali la 41 kwa Usahihi


SWALI LA 41
Fursa uzalendo ktk nchi yako
Kukatoa rushwa ktk nchi hii ya Tanzania

**Kielelezo Na. 1.2 (b)**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyeshindwa Kujibu Swali la 41 kwa Usahihi

**Swali la 42**: Pazi ni mwanafunzi mwenye tabia ya kukiuka sheria za shule. Je, ni madhara gani mawili yanaweza kumpata ?

Swali hili lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa Mwajibikaji* na liliwataka watahiniwa kubainisha madhara ya kukiuka sheria za shule. Swali lilifanywa na watahiniwa 1,356,306 kati ya hao 860,269 (63.42%) walipata alama 1 hadi 2 na watahiniwa 496,037 (36.57%) walipata 0. Chati Na. 42 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 42.





**Chati Na. 42**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 42*

Watahiniwa 450,755 (33.23%) waliopata alama 2 walijua kuwa sheria za shule zina jukumu muhimu katika kudumisha mazingira salama, yenye tija na yenye utaratibu wa kujifunzia. Sheria za shule huhakikisha usalama, ustawi, na ukuaji wa elimu wa wanafunzi. Zaidi ya hayo, ni muhimu kwa wanafunzi kutii sheria na kanuni za shule kwa sababu zinahakikisha utaratibu na nidhamu, umakini wa kitaaluma, heshima, usalama, uwajibikaji na ustaarabu, maandalizi ya siku zijazo na ukuaji wa binafsi. Kutozitii kunaweza kusababisha kupoteza uaminifu, hatua za kinidhamu, utendaji duni wa kitaaluma, matokeo mabaya ya kijamii, maendeleo ya tabia mbaya, matokeo ya kisheria na athari juu ya kujithamini.

Watahiniwa waliotaja *kufanya vibaya kimasomo* walifahamu kuwa kutotii sheria za shule kunaweza kusababisha utoro wa mara kwa mara miongoni mwa wanafunzi, kuadhibiwa mara kwa mara kwa kupangiwa kazi nje ya

darasa, jambo ambalo husababisha kupoteza muda zaidi kwa mambo yasiyo ya kitaaluma na kushindwa kufanya vizuri kitaaluma. Vile vile, baadhi ya watahiniwa walibainisha hatua zinazosimamiwa kama jibu na kikwazo kwa kitendo au tabia fulani isiyofaa au isiyokubalika. Hawa walifahamu kuwa wanafunzi wanaokiuka sheria za shule wanaweza kukabiliwa na adhabu mbalimbali kama vile kusimamishwa shule, viboko au kupangiwa kazi za ziada. Vilevile, waliotaja *kufukuzwa shule* walifahamu kuwa kila mwanafunzi analazimika kutii sheria za shule vinginevyo kujihusisha na makosa makubwa ambayo yanaleta machafuko shuleni kama vile kususia masomo na mapigano kati ya wanafunzi kunaweza kusababisha kufukuzwa shule.

Vilevile, *kupoteza uaminifu*, ambayo inarejelea upotezaji wa sifa muhimu za kutegemewa kama waaminifu au wakweli, ilitolewa na watahiniwa ambao walielewa athari za ushiriki wa mara kwa mara wa wanafunzi katika kukiuka sheria za shule kwamba ni sawa na kupoteza uaminifu miongoni mwa wanafunzi wenzao na pia walimu. Wakati tabia hii ikiendelea, mwanafunzi anakuwa si mwaminifu na asiyetabilika. Kielelezo Na. 2.1 Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kujibu vizuri swali la 42.


SWALI LA 42

i) Anaweza kuachishwa shule
ii) Anaweza kufeli mtihani yake

**Kielelezo Na. 2.1**: *Sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali la 42 kwa usahihi*

Katika Kielelezo Na. 2.1, mtahiniwa aliandika madhara yanayoweza kumpata mwanafunzi mwenye tabia ya kukiuka sheria za shule.

Vilevile, watahiniwa 409,514 (30.19%) waliopata alama 1 walikuwa na uelewa wa wastani kuhusu madhara ya ukiukaji wa sheria za shule. Kwa hiyo, majibu yao yalikuwa na mchanganyiko wa majibu sahihi na yasiyo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika jibu lisilo sahihi ambalo ni *Tabia zisizozingatia maadili*. Hili lilihusiana na aina za tabia na linamaanisha vitendo visivyofaa ambavyo vinasigana na viwango vya kimaadili viliyowekwa na jamii fulani. Mfano wa vitendo hivi ni pamoja na kuiba, kusema uongo na kutumia lugha ya kuudhi. Mchanganyiko

mwingine wa majibu ulijumuisha majibu yasiyo sahihi kama vile, *Kundi rika na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya*. Kundi rika linamaanisha kundi la watu walio katika kundi moja la umri na matumizi mabaya ya madawa ya kulevya ni kitendo kisichofaa cha matumizi ya madawa ya kulevya kwa sababu zisizo za kitabibu ambayo husababishwa na mambo mbalimbali kama kushindwa kuhimili ushawishi wa makundi rika. Vilevile, ufaulu wa baadhi ya watahiniwa uliathiriwa na kurudia hoja, kwa mfano, mtahiniwa aliandika *Kutokufaulu vizuri* na *Kutofanikiwa katika elimu* kama hoja mbili zinazojitegemea ilihali zinaongelea hoja moja ya Ufaulu duni kitaaluma. Vivyo hivyo, mtahiniwa mwingine aliandika hoja mbili zinazofanana zilizohusiana na athari za kupoteza sifa ya kuwa mwaminifu na mkweli kwa kuzifanya hoja mbili tofauti. Hoja hizo ni *Kuchukiwa na walimu* na *kutopendwa na wanafunzi*. Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa waliandika hoja pungufu ya zilizohitajika. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika hoja moja tu ambayo ni *Kutofaulu mitihani* na mwingine aliandika *Kufukuzwa shule moja kwa moja* kama hoja pekee kwa swali hili. Kutokana na kasoro hizo, majibu ya watahiniwa katika kipengele hiki, hayakustahili zaidi ya alama 1.


Kwa upande mwingine, watahiniwa 496,037 (36.57%) waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa kuhusu madhara ya ukiukaji wa sheria za shule na walishindwa kubaini matakwa ya swali. Watahiniwa walioshindwa kuelewa matakwa ya swali walibainisha sababu mbalimbali zinazosababisha watu kutenda matendo yasiyofaa kwa kutaja hoja kama vile, *Kukosa Uadilifu, Kukosekana Kwa Uwazi, Kukosa Uaminifu, Kukosa uzalendo* na *Kutowajibika*. Vivyo hivyo, baadhi ya watahiniwa walieleza hoja zinazohusiana na matendo yanayoashiria kuwajali na kuwathamini watu wengine katika jamii. Kwa mfano, watahiniwa wawili waliandika *Kuwaheshimu wengine, Kusaidia watu wengine, Kuzungumza nao* na *Kuwasaidia*. Majibu haya kiuhalisia yanahusisha matendo ya kimaadili ambayo mtu anatakiwa kutendewa kuliko kuadhibiwa. Matendo haya hayavunji sheria za shule bali yanasaidia utekelezaji wa sheria kwa kuwa yanatengeneza mahusiano mazuri kwa walimu na wanafunzi. Dhana potofu nyingine ni watahiniwa wengine kuhusianisha madhara ya kutotii sheria za shule na kukosa utiifu kwa sheria za nchi kwa kuandika hoja kama vile *Kufungwa jela na kunyongwa,* na *Kupelekwa mahakamani*. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha taratibu za kusimamia na kuendesha shule ambazo zinaongozwa na taratibu na kanuni kinyume na masuala ya umma ambayo yanaongozwa na sheria za nchi zinazo

shughulikia makosa ya jinai. Sambamba na hao, watahiniwa wengine walitaja madhara ya kukiuka sheria za usalama barabarani kwa kutaja hoja kama vile *Kujeruhiwa* na *Kupata ajali ya pikipiki*. Pia, mwingine aliandika *Magari Kuharibika* na *Kukamatwa na askari wa usalama barabarani*.


Vilevile, watahiniwa wengine walitafsiri vibaya matakwa ya swali na tabia mbalimbali zisizofaa ambazo kwa namna moja au nyingine mwanafunzi akiwa nazo husababisha kuadhibiwa kwa sababu zinakiuka sheria za shule. Hao walitaja hoja kama vile *Kuwa wezi, Kuwa mtoro, Kupigana, Utovu wa nidhamu, Matumizi ya madawa ya kulevya, Kujiunga na makundi hatarishi* na *Ukabaji*. Katika mwelekeo huo huo, baadhi ya watahiniwa walikiuka matakwa ya swali kwa kuandika madhara ya kuwa na tabia mbaya kwa mfano, *Mwanafunzi kupata mimba ya utotoni, Kupata magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya ngono, Kunyanyaswa kingono*, *Kukosa maarifa na ujuzi* na *Kifo.*

Vivyo hivyo, watahiniwa wengine waliandika majibu yasiyohusiana na swali ambayo yaliendana na vyeo mbalimbali vya uongozi wa shule na serikali ya wanafunzi kama vile, *Mwalimu wa nidhamu, Mwalimu Mkuu, Kaka Mkuu* na *Kiranja wa nidhamu*. Majibu kama hayo yanahitimisha kuwa watahiniwa walishindwa kutofautisha matokeo ya kukiuka sheria za shule dhidi ya watu waliokuwa na nafasi za kudumisha nidhamu shuleni. Pia, baadhi ya watahiniwa hawakuzingatia mawanda ya swali kwa kujadili madhara yanayoweza kumpata mwanafunzi kwa kukiuka sheria za shule nje ya mazingira ya shule. Mfano, baadhi yao waliandika hoja kama vile *Atakanwa na wazazi wake kwa sababu ya utukutu shuleni*, *Atachukiwa na watu katika jamii*, *Atachafua sifa ya shule.*

Zaidi ya hao, wapo watahiniwa ambao hawakuelewa swali hivyo walielezea stadi mbalimbali za maisha kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja stadi zifuatazo: *Kujielewa* na *Kujiamini*. Majibu mengine yasiyo sahihi yaliyotajwa na watahiniwa ni kama vile *Kuathirika kisaikolojia, Kujadiliana, Kukiuka sheria za shule, kuwa na nidhamu, tabia njema, Kuwa na akili* na *Kujiheshimu*. Kwa ujumla, watahiniwa wengi hawakuwa na maarifa juu ya umahiri husika. Vielelezo Na.2.2 (a) na (b) ni sampuli ya majibu ya watahiniwa walioshindwa kujibu kwa usahihi swali la 42.


SWALI LA 42 (i) Kuwa mwizi
(ii) Ukosefu wa nidhamu kwa walimu na wazazi

**Kielelezo Na. 2.2:** (a) *Sampuli ya Majibu yasiyo sahihi ya swali la 42*



SWALI LA 42
i) Kuvuta Sigara
ii) Kuwa mwizi

**Kielelezo Na. 42.2:** **(b)** *Sampuli ya Majibu yasiyo sahihi ya swali la 42*

Katika ***Vielelezo Na. 42.2 (a) na (b)***, watahiniwa hawakuweza kubainisha athari anazoweza kupata mwanafunzi kwa kukiuka sheria za shule badala yake waliorodhesha matendo yanayoathiri mahusiano mazuri katika jamii.

**Swali la 43**: Vyanzo gani viwili vinaweza kutumika kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni?

Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa kuwa mwajibikaji na liliwataka watahiniwa kubainisha vyanzo vinavyotumika kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 na uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 46,072 (3.40%) walipata alama 1 hadi 2 na watahiniwa 1,310,234 (96.60%) hawakujibu kwa usahihi. Chati Na. 43 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 43.





**Chati Na. 43**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 43*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 5,164 (0.38%) waliopata alama 2 waliweza kubainisha vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni. Watahiniwa hawa walikuwa wanajua ulazima wa kutoa taarifa kutoka kwenye uongozi wa shule kwenda kwa wanafunzi na kutoka kwa wanafunzi kwenda kwenye utawala au uongozi wa shule. Mtahiniwa mmoja alibainisha njia mbili ambazo ni *ubao wa matangazo* na *matangazo ya paredi*. Mtahiniwa huyu alikuwa anajua kuwa ubao wa matangazo hutumika kutoa taarifa na maelekezo kwa wanafunzi, walimu na jumuiya nzima ya shule. Hivyo, humfanya mwanafunzi kupata taarifa za kila mara kuhusu mambo mbalimbali, kama vile matukio, ratiba, fursa mbalimbali, matokeo, bajeti ya shule na matumizi. Vilevile, mtahiniwa huyu alikuwa anaelewa kuwa walimu na wanafunzi hukusanyika paredi hasa muda wa asubuhi kama maandalizi ya kuanza masomo kwa siku hiyo. Wakiwa paredi, walimu hutoa matangazo, nasaha na maneno ya kuwatia moyo wanafunzi. Pia, wanafunzi hupata fursa ya kutoa neno kwa wanafunzi wenzao. Aidha, paredi ni moja ya sehemu inayokuza stadi kwa mwanafunzi kujieleza na kuzungumza kwenye hadhara.

Mtahiniwa mwingine aliandika ubao wa matangazo na baraza la shule. Mtahiniwa huyu alikuwa sahihi kwa sababu baraza la shule ni mkutano wa walimu na wanafunzi shuleni, na mara nyingi hufanyika wakati wa kuanza

au kumaliza muhula kwa lengo la kutoa taarifa mbalimbali. Baraza la shule linaweza kuhusisha sala na maombi, taarifa, mijadala, ushauri, mikakati ya shule na kutoa zawadi kwa vanafunzi waliofanya vizuri katika vipengele mbalimbali. Kwa ujumla, njia nyingine ni pamoja na matangazo ya asubuhi, ubao wa matangazo na matangazo ya darasani. Kielelezo Na. 3.1 Ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini vyanzo vinavyoweza kutumika kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni.


SWALI LA 43

i) Ubao wa matangazo wa shule.

ii) Paredi ya asubuhi shuleni.

***Kielelezo Na. 3.1****: Sampuli ya Majibu Sahihi Kutoka kwa Mtahiniwa Aliyejibu Swali la 43*

Katika Kielelezo Na. 3.1, Mtahiniwa aliweza kubaini vyanzo vinavyoweza kutumika kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni.

Hata hivyo, watahiniwa 40,908 (3.02%) waliopata alama 1 hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya vyanzo sahihi vya kupokea na kutoa taarifa shuleni. Baadhi ya watahiniwa walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi. Mathalani, mtahiniwa mmoja aliandika *matangazo ya paredi* na *ndani ya darasa*. Mtahiniwa huyu hakujua kwamba darasa ni chumba/sehemu shuleni ambako mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hufanyika.

Mtahiniwa mwingine alijibu kwa kutaja *ubao wa matangazo* na *kiranja wa darasa* kama vyanzo vya kutoa na kupokea taarifa sahihi shuleni. Kadhalika, mtahiniwa huyu hakujua kuwa wajibu wa kiranja wa darasa ni kuimarisha nidhamu ya wanafunzi, kuhakikisha darasa lipo kwenye utaratibu, kusimamia rasilimali za darasa, kuhakikisha mazingira ya darasa ni tulivu kwa ajili ya zoezi la ufundishaji na ujifunzaji.

Vilevile, mtahiniwa mwingine katika kundi hili alitaja *baraza la shule* na *sanduku la maoni* kama vyanzo vya kupokea na kupata taarifa sahihi

shuleni. Mtahiniwa huyu hakujua kuwa sanduku la maoni ni sanduku maalumu linalowekwa kwenye mazingira ya shule kwa ajili ya wanafunzi kuweka maoni, mawazo, ushauri na malalamiko kwa usiri. Sanduku la maoni sio chanzo cha taarifa sahihi kwa sababu taarifa hutolewa kwa siri. Aidha, katika kundi hili kuna watahiniwa waliorudia hoja. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *ubao wa matangazo* na *kubandika matangazo* kama hoja mbili tofauti wakati matangazo hubandikwa kwenye ubao wa shule hivyo kupata alama 1.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,310,234 (96.60%) waliopata 0 kwenye swali hili walishindwa kutambua matakwa ya swali na wengine hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa shuleni. Kwa mfano, baadhi ya watahiniwa waliandika baadhi ya sifa za mtu anayetoa taarifa sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja *uaminifu na uadilifu*, na mwingine aliandika *kuwa mkweli na kuzingatia maadili*. Watahiniwa hawa hawakuelewa kwamba kuwa na uaminifu na maadili sio vyanzo vya taarifa shuleni bali ni sifa muhimu za mtu yeyote mwenye kutoa taarifa zenye ukweli.

Vilevile, kuna watahiniwa waliohusisha vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa sahihi na aina za mawasiliano. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja *kwa kuongea* na *kutotumia sauti*, na mwingine aliandika *kutumia alama* na *kutumia maandishi* kama misingi ya kupokea na kutoa taarifa sahihi. Aidha, kuna lugha ya alama ambayo hutumiwa na viziwi katika kuwasiliana. Vile vile, mawasiliano kwa maandishi yanayohusisha njia kama vile barua, barua pepe na nyaraka mbalimbali ambazo zinaweza kuwa katika muundo wa nakala ngumu au tepe. Pia, watahiniwa hawakujua kuwa mawasiliano ya kutumia sauti hufanyika kwa kutumia mdomo, na yanaweza kufanyika kwa kutumia simu au kuonana. Kwa ujumla, aina za mawasiliano haziwezi kutumika kama chanzo cha kupokea au kutoa taarifa sahihi.


Halikadhalika, kuna watahiniwa ambao walishindwa kubaini matakwa ya swali, hivyo kutaja njia zinazotumika kupokea na kutoa taarifa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *simu* na *barua pepe* na mwingine aliandika *barua pepe* na *barua*. Mtahiniwa huyu hakujua kwamba simu, barua na barua pepe hutumika kutuma ujumbe kati ya mtu na mtu hivyo sio vyanzo vya taarifa katika mazingira ya shule.

Aidha, watahiniwa wengine walikwenda mbali zaidi kwa kupendekeza matukio yasiyo ya kawaida yanayotokea shuleni. Mfano, kutoa taarifa panapokuwa na matukio yasiyo ya kawaida shuleni. Kwa mfano, changamoto mbalimbali zinazojitokeza baina ya wanafunzi, kama vile: *wanafunzi wakiwa na matatizo, wanafunzi wakikosa nidhamu, wakichora ukuta, wanafunzi washindwa mitihani* na *wanafunzi wakiugua*. Watahiniwa hawa hawakujua kuwa matatizo yanayohusiana na wanafunzi sio vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa kwani matatizo hayo yanaweza kutatuliwa kupitia taratibu maalumu za uongozi wa shule.

Vilevile, uchambuzi uliofanyika kwenye majibu ya watahiniwa ulibaini kuwa kuna watahiniwa waliotaja watu mbalimbali ambao hutoa matangazo shuleni kama vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja *aliandika mwalimu mkuu* na *mwalimu wa zamu*. Watahiniwa hawa walishindwa kutofautisha kati ya vyanzo vya kutoa na kupokea taarifa na muundo wa uongozi wa shule. Mwalimu mkuu, mwalimu wa darasa, mwalimu wa zamu, na kiranja mkuu huunda muundo kamili wa uongozi wa shule. Kila kiongozi ana jukumu lake maalumu katika kuhakikisha uendeshaji wa shule unaenda vizuri. Moja ya jukumu la uongozi wa shule ni kusaidia upokeaji na upashaji habari ili malengo ya shule yafikiwe.

Aidha, kuna watahiniwa walioshindwa kubaini matakwa ya swali, badala yake wakaeleza alama mbali mbali zinazoitambulisha shule kama vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa. Mathalani, mtahiniwa mmoja alitaja *nembo ya shule* na *wimbo wa shule*. Watahiniwa hawa hawakujua kuwa alama kama nembo ya shule, wimbo, sare na kaulimbiu hutumika kuitambulisha shule.

Mwisho, kuna watahiniwa waliobainisha mitandao ya kijamii kama vyanzo vya kupokea na kutoa taarifa shuleni. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *Instagram* na *facebook* na mwingine alitaja *WhatsApp* na *Twitter.* Watahiniwa wengine walitaja *ngoma, baragumu* na *pembe* ambazo ni njia za asili za kutoa taarifa. Watahiniwa hawa hawakuwa sahihi kwa sababu mitandao ya kijamii sio njia rafiki ya mawasiliano baina ya uongozi wa shule na wanafunzi wakiwa shuleni. Pia, wanafunzi hawaruhusiwi kutumia simu wakiwa shuleni, na nyumbani; na kama zikitumika, hutumika chini ya uangalizi wa wazazi au walezi. Vielelezo Na. 3.2 (a) na (b) vinaonesha watahiniwa walioandika majibu yasiyo sahihi.




SWALI LA 43

i) Kuepuka ngono

ii) Wizi wa rasilimali za Shule

**Kielelezo Na. 3.2 (a)**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa katika swali la 43*



SWALI LA 43

i) Kuwa mwaminifu


ii) Kujiamini

**Kielelezo Na. 3.2 (b)**: *Sampuli ya majibu yasiyo sahihi kutoka kwa mtahiniwa katika swali la 43*

Katika Kielelezo Na. 3.2 (b): Mtahiniwa hakuweza kutaja vyanzo vinavyoweza kutumika kupokea na kutoa taarifa sahihi shuleni, hivyo akaandika sifa za mwanafunzi mwenye nidhamu.

**Swali la 44**: Njia zipi mbili zinaweza kutumika kuondoa changamoto ya miundombinu chakavu na mrundikano wa kesi mahakamani kwa lengo la kusaidia mahakama kufikia malengo yake?

Swali lilitungwa kutoka katika umahiri mkuu wa *Kuwa mwadilifu* na lilimtaka mtahiniwa kubainisha njia zinazoweza kutumika kuondoa changamoto ya miundombinu chakavu na mrundikano wa kesi mahakamani. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 ambapo watahiniwa 312,784 (23.06%) pekee walipata alama 1 hadi 2 na watahiniwa 1,043,522 (76.94%) walipata 0. Chati Na. 44 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 44.





**Chati Na. 44**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 44*

Uchambuzi uliofanyika katika majibu ya watahiniwa unaonesha kwamba watahiniwa 50,746 (3.74%) waliopata alama zote na walielewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja, *kuboresha miundombinu kama vile kujenga majengo mapya* na *kutoa elimu kwa raia ili wapunguze kufanya maovu*. Mtahiniwa huyu alikuwa anajua kuwa ujenzi wa mahakama kwa ngazi zote, ikiwa ni pamoja na mahakama za mwanzo, wilaya unasaidia kupatikana kwa huduma ya mahakama karibu na wananchi na kwa gharama nafuu. Pia, watahiniwa walifahamu kuwa ujenzi wa vituo jumuishi vya utoaji haki ambavyo vitatoa huduma kuanzia mahakama ya mwanzo hadi ya rufaa vitasaidia wananchi kupata huduma mbalimbali za kisheria na kuokoa muda wa kuendesha kesi na gharama. Aidha, mtahiniwa huyu alikuwa na uelewa kwamba jamii ikielimishwa na kuacha kufanya maovu na kufuata sheria, mrundikano wa kesi mahakamani utapungua.

Mtahiniwa mwingine alitaja kuajiri *wafanayakazi wa mahakama kama vile mahakimu na wasio mahakimu* na kutumia teknolojia ya kisasa ili kurahisisha *michakato mbalimbali ya mahakama*. Mtahiniwa huyu alielewa kuwa rasilimali watu kama vile majaji, mahakimu na wafanyakazi wengine wanahitajika ili kuwepo uwiano wa kesi na wafanyakazi mahakamani. Aidha, upatikanaji wa teknolojia, hasa matumizi ya vifaa vya Teknolojia ya

Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa maofisa wa mahakama na askari polisi utarahisisha upelelezi, usikilizwaji wa kesi, mashtaka na utunzaji wa kumbukumbu za kesi. Vilevile, wanaelewa changamoto nyingine za mahakama ikiwa ni pamoja na mrundikano wa kesi, rasilimali chache, rushwa, ukosefu wa uelewa wa kisheria, miundombinu duni, uzembe na taratibu za polepole. Kielelezo Na. 4.1 Ni sampuli ya majibu sahihi ya mtahiniwa katika swali la 44.


SWALI LA 44 Njia zinazoweza kutumika kuondoa changamoto hiyo ni
@ Kujenga mahakama mpya na miundombinu inayohitajika
ⓑ Kupata wafanyakazi wa kutosha mahakamani yaani Mahakimu wa kusikiliza kesi

***Kielelezo Na. 4.1**: Sampuli ya Majibu Sahihi ya Mtahiniwa Katika Swali la 44*

Katika kielelezo 4.1, Mtahiniwa aliandika njia mbili zinazoweza kutumika kuondoa changamoto ya miundombinu chakavu na mrundikano wa kesi mahakamani.

Vilevile, watahiniwa 262,015 (19.32%) waliopata alama 1 walikuwa na udhaifu mbalimbali kama vile kuandika hoja kwa kuzirudia rudia. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kuajiri mahakimu wengi* na *kusomesha makarani wa mahakama* kama hoja mbili tofauti wakati zote zinalenga kuboresha hali ya rasilimali watu kwenye mfumo wa mahakama. Mfano mwingine, ni mtahiniwa aliyeandika *kujenga mahakama mpya* na *kukarabati majengo ya mahakama* kama hoja mbili tofauti wakati zote zina shabaha ya kuboresha miundombinu. Halikadhalika, kuna watahiniwa walioandika hoja moja tu badala ya mbili kinyume na swali lilivyotaka. Mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kuisaidia mahakama iwe na teknolojia ya habari na mawasiliano ili kurahisisha shughuli za mahakama*.

Aidha, kuna watahiniwa waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kuajiri mahakimu na majaji wengi* kama hoja ya kwanza, kisha *kusomesha walimu wa kutosha*. Mwalimu ni mtu anayewafundisha wanafunzi kupata maarifa, ujuzi na maadili. Mtahiniwa

mwingine alitaja *kutoa elimu kwa raia ili wapunguze kufanya makosa* ambalo ni jibu sahihi


Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha watahiniwa 1,043,522 (76.94%) waliopata 0 hawakuwa na maarifa kuhusu njia zinazoweza kutumika kuondoa chanagamoto ya miundombinu chakavu na pamoja na mrundikano wa kesi mahakamani. Walishindwa kutafsiri matakwa ya swali hivyo wakaandika mambo yasiyohusiana. Baadhi ya watahiniwa walihusianisha swali kimakosa na wajibu wa raia katika kukuza demokrasia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja *kuhudhuria mikutano ya hadhara* na *kupiga kura kuchagua viongozi* akiwa na maana ya njia ya kuboresha miundombinu ya mahakama na mrundikano wa kesi mahakamani. Mtahiniwa huyu hakujua kuwa kushiriki katika chaguzi kwa kupiga kura kunasaidia kukuza demokrasia na sio suluhu ya kuboresha mifumo ya mahakama. Vivyo hivyo, watahiniwa wengine walijikita kwenye sifa za raia mwema. Mathalani, mtahiniwa mmoja alitaja *kuwa mzalendo na kuwa mwadilifu*. Mtahiniwa huyu hakuelewa kwamba mtu kuwa mwaminifu na anaipenda nchi yake haina maana kwamba ana lengo la kuboresha huduma za mahakama. Uzalendo na uadilifu hulinda maslahi ya taifa, husaidia kupambana na rushwa, kudumisha amani na ustawi wa taifa kwa ujumla.

Aidha, kuna watahiniwa waliofananisha dhana ya miundombinu ya mahakama na miundombinu ya usafirishaji. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza *uboreshaji wa barabara* na *uboreshaji wa reli*. Mwingine alipendekeza *ujenzi wa meli* mpya na *ununuzi wa ndege mpya*. Watahiniwa hawa hawakuelewa matakwa ya swali kwani uboreshaji wa njia za usafirishaji unasaidia ukuaji wa uchumi kwa kurahisisha usafirishaji wa abiria, mali ghafi, bidhaa na huduma. Kadhalika kuna watahiniwa waliopendekeza njia mbalimbali za kukusanya fedha kwa ajili ya kukarabati miundombinu ya mahakama. Mtahiniwa mmoja kwa mfano alishauri *kuita watu kwa ajili ya harambee* na *kuwaomba nchi wahisani*, mwingine alishauri *watu wajitolee kutoa fedha* na *kuhakikisha watu wanatoa kodi*. Watahiniwa hawa hawakujua kuwa uwepo wa fedha sio suluhisho la moja kwa moja kwa changamoto zinazoikumba mahakama endapo utatuzi wake hautapewa kipaumbele.

Vilevile, kuna watahiniwa waliopendekeza njia ambazo ni za kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani ambazo hazifai kwani njia hizo zikizingatiwa zinaweza kuathiri utengamano katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kuacha kufikisha watuhumiwa mahakamani* na *kupiga watuhumiwa mtaani*. Mtahiniwa mwingine aliandika *watu wavumilie wakiona maovu*. Kwa upande mwingine, kuna watahiniwa waliokwenda mbali zaidi wakapendekeza kuanza kutumia utawala wa kidikteta kama suluhu ya kupunguza mrundikano wa kesi mahakamani. Mathalani, kuna mtahiniwa aliyeandika *kutumia utawala wa kidikteta*. Watahiniwa hawa hawakuelewa sifa za utawala wa kidikteta kwamba ni utawala ambao hauzingatii utawala wa sheria; haki za binadamu hivyo hauwezi kuwa suluhisho kwa changamoto zinazoukumba mfumo wa mahakama.

Aidha, kuna watahiniwa waliopendekeza serikali iingie ubia na sekta binafsi katika kuendesha mfumo wa mahakama. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza *majengo ya mahakama yabinafsishwe* na *tukaribishe wawekezaji* akiwa na maana njia za kuboresha utendaji wa mfumo wa mahakama. Watahiniwa hawa walikwa hawajui kuwa mahakama ni moja kati ya mihimili mitatu ya dola, kwa hiyo haiwezi kubinafsishwa. Mahakama inatafsiri sheria, inatoa haki sawa kwa raia na inasikiliza na kuamua kesi mbalimbali.


Mwisho, kuna watahiniwa waliotoa mchanganyiko wa hoja ambazo hazihusiani na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alipendekeza *kujenga vituo vya polisi* na *kujenga magereza*. Mwingine alishauri *kila mtu awe na ulinzi binafsi* na *kuhakikisha usalama barabarani.* Na mtahiniwa mwingine alipendekeza *kutoa elimu juu ya namna ya kukarabati miundombinu* na *kutoa ushauri nasaha kwa wale wenye kesi mahakamani*. Aidha, kuna watahiniwa ambao hawakufanya hili swali kabisa. Vielelezo na. 4.2 (a) na (b) vinaonesha majibu ya watahiniwa yasiyo sahihi katika swali la 44


SWALI LA 44

a) Kuweka sheria za barabarani

b) Kuwa na serikali za mitaa

**Kielelezo Na. 4.2:** *(a) mtahiniwa aliandika hoja ambazo haziendani na hitaji la swali*





**Katika kielelezo Na.4.2**: *(b) Mtahiniwa aliandika hoja ambazo haziendani na hitaji la swali*

Katika Kielelezo Na. 4.2. (a) na (b) Watahiniwa hawakuweza kubainisha njia zinazoweza kutumika kuondoa changamoto ya miundombinu chakavu na mrundikano wa kesi mahakamani badala yake waliandika mambo ambayo hayahusiani na hitaji la swali.

**Swali la 45**: Kwa nini jumuiya za kiuchumi katika bara la Afrika hazijafikia malengo yaliyotarajiwa? Toa sababu mbili.


Swali hili lilitoka katika umahiri mkuu wa *Kudumisha Amani* na lilipima uwezo wa watahiniwa kubaini sababu zinazosababisha jumuiya za kiuchumi barani Afrika kutokufikia malengo yaliyotarajiwa. Swali lilijibiwa na watahiniwa 1,356,306 kati ya hao watahiniwa 574,642 (42.37%) walipata alama kuanzia 1 hadi 2 na watahiniwa 781,664 (57.63%) walipata alama 0. Chati 45 inaonesha ufaulu wa watahiniwa katika swali la 45.




**Chati Na. 45**: *Ufaulu wa Watahiniwa Katika Swali la 45*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 236,575 (17.44%) walipata alama zote 2. Watahiniwa hawa walielewa Jumuiya za Kiuchumi kama mchakato wa nchi katika bara kuja pamoja ili kukuza ushirikiano wa kiuchumi. Jumuiya za kiuchumi zinakusudia kukuza biashara, ukuaji wa uchumi, ukuaji wa viwanda, maendeleo ya miundombinu na utulivu wa kisiasa. Baadhi ya faida za mtangamano ni kufanya biashara miongoni mwa nchi wanachama, kupanua soko la bidhaa zinazozalishwa katika nchi wanachama, kuimarisha usalama miongoni mwa nchi wanachama, kuboresha miundombinu na mawasiliano. Faida nyingine ni kukuza kilimo na maendeleo ya viwanda miongoni mwa nchi wanachama. Baadhi ya jumuiya hizo ni pamoja na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), na Jumuiya ya Kiuchumi ya Nchi za Afrika Magharibi (ECOWAS). Jumuiya za Kiuchumi zinategemewa kuhudumia nchi wanachama kwa kutekeleza ajenda za kikanda kwa nia njema kupitia mikataba iliyounda jumuiya ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Watahiniwa hao walifahamu sababu za kushindwa kwa jumuiya za Kiuchumi barani Afrika kufikia malengo yao kama vile kuwepo kwa vita vya *wenyewe kwa wenyewe, tofauti za viwango vya uchumi na umaskini, ubinafsi wa baadhi ya nchi wanachama, teknolojia duni, mtaji duni na utoaji duni wa elimu ya uraia kwa watu*. Walielewa kuwa mapambano kati ya makundi yaliyopangwa ndani ya kundi moja yanasababisha hasara kubwa ya kiuchumi katika suala la uharibifu wa majengo, miundombinu ya usafiri na mawasiliano, kupoteza maisha na kadhalika ambayo inapunguza michango ya nchi hizo katika maendeleo ya jumuiya. Ubinafsi wa baadhi ya viongozi wa serikali kwa maslahi yao binafsi badala ya yale ya kitaifa unadhoofisha mikakati ya jumuiya hizo kuelekea malengo yaliyowekwa. Aidha, watahiniwa hao walifahamu kuwa ukosefu wa teknolojia ya kisasa ambayo ingetumika kuboresha sekta ya kilimo, viwanda na madini unakwamisha jumuiya kufikia malengo yake. Vilevile, watahiniwa hao walielewa kuwa elimu kwa wananchi juu ya haki zao, wajibu kwa viongozi na kwa wananchi ingeingiza moyo wa uzalendo miongoni mwao na kutoa ushirikiano kwa ajili ya maendeleo ya jamii. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kubaini matakwa ya swali la 45.


SWALI LA 45

a) Vitavya wenyewe kwawenyewe
b) Tofautiza Itikadi

**Kielelezo Na. 5.1**: Sampuli ya Majibu ya Mtahiniwa Aliyejibu Swali la 45 kwa Usahihi.

Katika Kielelezo Na. 5.1, Mtahiniwa aliweza kueleza sababu mbili zinazofanya jumuiya za kiuchumi barani Afrika kutokufikia malengo yaliyotarajiwa.

Hata hivyo, watahiniwa 338,044 (24.92%) waliopata alama 1 walikosa uelewa wa kutosha juu ya sababu zinazosababisha jumuiya za kiuchumi barani Afrika kutokufikia malengo yaliyotarajiwa. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kwa sababu ya utofauti wa kibaiolojia ya watu katika nchi wanachama* na *kwa sababu ya kukosekana utulivu wa kisiasa au uwepo wa vita*. Jibu la kwanza lilihusiana na maswala ya utofauti wa kijinsia baina ya wanawake na wanaume na jibu la pili ni mojawapo ya majibu sahihi katika swali hili. Mtahiniwa mwingine aliyechanganya majibu aliandika *maendeleo duni ya kiuchumi kwa baadhi ya nchi za Afrika* na nchi *za Afrika ziko chini ya utawala wa kikoloni*.


Aidha, watahiniwa wengine walirudia hoja, kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika *kwa sababu ya kukosekana kwa utulivu wa kisiasa katika nchi za Afrika* na *uwepo wa vita za wenyewe kwa wenyewe.* Mtahiniwa mwingine katika kundi hili, aliandika *uchumi mbovu kwa baadhi ya nchi za kiafrika* na *umasikini baina ya nchi za kiafrika* kama hoja mbili tofauti.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 781,664 (57.63%) waliopata alama 0 walishindwa kutafsiri matakwa ya swali, na wengine walikosa uelewa wa sababu zinazosababisha jumuiya za kiuchumi barani Afrika kutofikia malengo yaliyotarajiwa. Kwa mafano, mtahiniwa mmoja alieleza mambo yanayohusiana na njia za kupambana na rushwa katika nchi kama vile *kuwa mzalendo* na *kuwa mwaminifu*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa kuipenda na kuwa tayari kuifia nchi yako ni muhimu kwa ustawi wa nchi au taifa na sio jumuiya za kikanda. Pia, watahiniwa hawakulielewa swali kwa

kuhusisha dhana ya kuwa mwaminifu ambayo ni hali ya kuwa mkweli na changamoto za jumuiya za kiuchumi barani Afrika. Hivyo, majibu hayo hayakuendana na swali lililoulizwa. Vilevile, watahiniwa wengine walieleza sheria na kanuni mbalimbali za kuandaa mpango kazi wa shule. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika kuzingatia *muda wakati wa utekelezaji wa malengo ya shule* na *kufanyia kazi malengo ya shule yaliyowekwa*. Watahiniwa hao hawakuelewa kuwa jumuiya za kiuchumi zinahusisha umoja wa nchi kadhaa na sio katika ngazi ya shule.


Aidha, baadhi ya watahiniwa walieleza mambo ya msingi kwa nchi kuendelea, kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika *uwepo wa amani katika nchi* na *uwepo wa ulinzi katika nchi*. Walishindwa kuelewa kuwa jumuiya za kiuchumi zinahusisha nchi Zaidi ya moja. Ni wazi kuwa majibu haya yangechochea zaidi ushirikiano na sio sababu za kushindwa kwa jumuiya. Watahiniwa wengine waliandika mataifa yaliyokuwa yakitawala nchi za Afrika. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika *kwa sababu nchi za kiafrika zilikuwa chini ya utawala wa mwingereza* na *kwa sababu nchi za Afrika zilipata uhuru kwa njia ya vita*. Wengine walienda mbali zaidi kwa kuhusianisha kutofikiwa kwa malengo ya jumuiya za kiuchumi na imani potofu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika kwa *sababu ya matendo ya kishirikina miongoni mwa waafrika*.

Watahiniwa wengine waliandika mambo ambayo hayakuhusiana na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika *kwa ajili ya kupinga* na *Kupigania haki zao*. Na mwingine aliandika *kwa sababu hazina sheria yoyote, hazina ruhusa za Baraza la Afrika*. Majibu yote haya yanadhihirisha uwezo wa watahiniwa wa kutokuwa na umahiri unaohusiana na masuala ya kimataifa. Vielelezo Na. 5.2 (a) na (b) vinaonesha sampuli ya majibu yasiyo sahihi katika kujibu swali la 45.


SWALI LA 45

(i) Kwa sababu hazina sheria yoyote
(ii) Kwa sababu hazina ruhusa za ~~Serikali~~ Baraza la Afrika.

**Kelelezo Na. 5.2**: (a) Sampuli ya Majibu Yasiyo sahihi kwa swali la 45.


SWALI LA 45

i/ KWAAJILI YA KUPINGA

ii/ KUPIGANIA HAKI ZAO

**Kelelezo Na. 5.2**: (b) Sampuli ya Majibu Yasiyosahihi kwa Swali la 45

## 3.0 HITIMISHO

Takwimu za uchambuzi zinaonesha kuwa umahiri wa aina sita ulitahiniwa mwaka 2023, ufaulu wake ulikuwa na wastani wa asilimia 53.37. Umahiri uliotahiniwa ni *Kuheshimu jamii, Kuithamini jamii, Kuwa mwajibikaji, Kuwa mstahimilivu, Kuwa mwadilifu* na *Kudumisha amani.* Mwaka 2022 umahiri uliotahiniwa ulikuwa na ufaulu wa wastani wa asilimia 56.3.

Uchambuzi wa takwimu unaonesha kuwa watahiniwa walikuwa na ufaulu mzuri katika umahiri wa *Kuithamini Jamii* (67.62%). Umahiri wa *Kuwa Mstahimilivu* ulikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu *(54.18%), Kuheshimu Jamii (54.03%), Kuwa Mwajibikaji* (51.05%), *Kudumisha Amani* (48.53%) na *Kuwa Mwadilifu* (44.81%).

Ulinganifu wa ufaulu wa umahiri uliotahiniwa katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi (PSLE) kwa mwaka, 2022 na 2023 unaonesha kuwa ufaulu wa umahiri wa *Kuithamini Jamii* kwa mwaka 2022 ulikuwa mzuri (68.40%) sawa na mwaka 2023 (67.62%). Umahiri wa *Kuwa Mwajibikaji* ufaulu ulikuwa mzuri (64.33%) kwa mwaka 2022 na wastani (51.05%) kwa mwaka 2023.

Ufaulu wa aina nyingine wa umahiri ulikuwa wa wastani ambapo, umahiri wa *Kudumisha Amani* ulikuwa (51.96%) mwaka 2022 na mwaka 2023 ulikuwa (48.53%). Umahiri wa *Kuheshimu Jamii* ufaulu wake ulikuwa wa wastani (53.77%) katika mwaka 2022 na (54.03%) katika mwaka 2023. Ufaulu wa *Kuwa mstahimilivu* ulikuwa wa wastani kwa mwaka 2022 (49.00%) na mwaka 2023 (54.18%). Aidha, ufaulu wa umahiri wa *Kuwa Mwadilifu* ulikuwa wa wastani (50.45%) mwaka 2022 pia kwa mwaka 2023 (44.81%).

## 4.0 MAPENDEKEZO

Ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa hususani katika umahiri wa *Kuthamini Jamii, Kuheshimu Jamii, Kuwa Mwadilifu na Kuwa Mvumilivu,* yafuatayo yanapendekezwa:

(a) Walimu watumie igizo dhima katika ufundishaji ili kuwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu katika kubaini matendo yenye kuheshimu jamii, kuithamini jamii na kudumisha amani katika jamii.

(b) Wanafunzi wasisitizwe kusoma vitabu vya kiada na ziada kwa bidii ili kuongeza maarifa na ujuzi katika dhana mbalimbali za Uraia na Maadili.

(c) Walimu watumie zana mbalimbali wakati wa ufundishaji na ujifunzaji kama vile michoro, ramani, chati, picha, video na majedwali kwani humvutia mwanafunzi kufuatilia kwa karibu ujifunzaji na kupata umahiri unaolengwa. Zana hizo zitamsaidia mwanafunzi kuhusianisha anachojifunza katika umahiri husika na mazingira halisi yanayomzunguka.

(d) Wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, walimu watumie zaidi mbinu shirikishi kama vile: majadiliano katika vikundi, matumizi ya hadithi fupi na majigambo, matumizi ya ziara za kimasomo, matumizi ya mbinu ya kualika wageni, midahalo na matumizi ya kazi mradi.

(e) Walimu waandae mazoezi na majaribio ya kutosha, na kutoa mrejesho ili kukuza uwezo wa wanafunzi kujibu maswali yanayoweza kupima stadi mbalimbali zinazopatikana katika umahiri wa *Kuthamini Jamii, Kuheshimu Jamii, Kuwa Mwadilifu na Kuwa Mvumilivu.*

*Kiambatisho*

**Ulinganifu wa Ufaulu kwa Watahiniwa kwa kila Umahiri katika Mtihani wa PSLE 2022 na 2023**

| Na | Umahiri | Mtihani wa 2022 | | | | Mtihani wa 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| 1. | Kuithamini Jamii | 9 | 55.43 | 68.4 | Vizuri | 9 | 55.17 | 67.62 | Vizuri |
| | | 10 | 77.2 | | | 10 | 82.66 | | |
| | | 12 | 73.38 | | | 11 | 56.34 | | |
| | | 13 | 72.34 | | | 12 | 51.86 | | |
| | | 14 | 51.37 | | | 13 | 17.99 | | |
| | | 42 | 80.7 | | | 22 | 79.71 | | |
| 2. | Kuwa Mwajibikaji | 15 | 68.68 | 64.33 | Vizuri | 15 | 12.84 | 51.05 | Wastani |
| | | 16 | 72.88 | | | 16 | 67.41 | | |
| | | 17 | 74.85 | | | 17 | 13.21 | | |
| | | 18 | 57.55 | | | 18 | 43.17 | | |
| | | 20 | 24.91 | | | 19 | 79.03 | | |
| | | 21 | 64.67 | | | 20 | 45.01 | | |
| | | 43 | 86.79 | | | 23 | 22.38 | | |
| | | | | | | 25 | 87.65 | | |
| | | | | | | 29 | 76.34 | | |
| | | | | | | 42 | 63.42 | | |
| 3. | Kuheshimu Jamii | 1 | 87.7 | 53.77 | Wastani | 1 | 32.16 | 54.03 | Wastani |
| | | 2 | 21.76 | | | 2 | 67.66 | | |
| | | 3 | 43.83 | | | 3 | 42.26 | | |
| | | 4 | 69.35 | | | 4 | 26.88 | | |
| | | 5 | 74.86 | | | 5 | 72.71 | | |
| | | 6 | 42.79 | | | 6 | 58.34 | | |
| | | 7 | 18.34 | | | 7 | 76.71 | | |
| | | 8 | 84.76 | | | 8 | 44.38 | | |
| | | 11 | 56.14 | | | 14 | 86.15 | | |
| | | 19 | 36.95 | | | 21 | 83.73 | | |
| | | 22 | 20.31 | | | 43 | 3.4 | | |

| Na | Umahiri | Mtihani wa 2022 | | | | Mtihani wa 2023 | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni | Ufaulu kwa kila Swali | | Wastani wa Ufaulu (%) | Maoni |
| | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | | Namba ya swali | (%) ya Ufaulu | | |
| | | 41 | 88.39 | | | - | - | | |
| 4. | Kudumisha Amani | 34 | 22.37 | 51.96 | Wastani | 35 | 14.99 | 48.53 | Wastani |
| | | 36 | 46.04 | | | 36 | 46.5 | | |
| | | 37 | 70.9 | | | 37 | 77.82 | | |
| | | 38 | 62.75 | | | 38 | 56.45 | | |
| | | 39 | 38.83 | | | 39 | 53.62 | | |
| | | 40 | 45.72 | | | 40 | 40.83 | | |
| | | 45 | 77.13 | | | 41 | 55.64 | | |
| | | | | | | 45 | 42.37 | | |
| 5. | Kuwa mwadilifu | 30 | 55.26 | 50.45 | Wastani | 32 | 62.74 | 44.81 | Wastani |
| | | 31 | 66.35 | | | 33 | 46.1 | | |
| | | 32 | 56.13 | | | 34 | 47.35 | | |
| | | 33 | 46.1 | | | 44- | 23.03 | | |
| | | 35 | 64.59 | | | | | | |
| | | 44 | 14.29 | | | | | | |
| 6 | Kuwa Mstahimilivu | 23 | 29.96 | 49 | Wastani | 24 | 59.95 | 54.18 | Wastani |
| | | 24 | 69.86 | | | 26 | 79.37 | | |
| | | 25 | 33.17 | | | 27 | 73.56 | | |
| | | 26 | 38.63 | | | 28 | 13.87 | | |
| | | 27 | 44.95 | | | 30 | 62.93 | | |
| | | 28 | 75.1 | | | 31 | 35.37 | | |
| | | 29 | 51.38 | | | | | | |